UCHANGANUZI WA TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA YA *PARADISO*: MTAZAMO WA KIDENGUZI

OCHARO FRANCINE


MA/KIS/ 1051146

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI NA MAWASILIANO KWENYE KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI YA KIJAMII, IDARA YA LUGHA, FASIHI NA MAWASILIANO, CHUO KIKUU CHA KIKATOLIKI CHA AFRIKA MASHARIKI

SEPTEMBA, 2026

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Saini:  Tarehe: 09/07/2026

OCHARO FRANCINE A.

Mtahiniwa (1051146)

IDHINI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki.

Saini:  Tarehe: 09/07/2026

Dkt. Mavisi Rose

Saini:  Tarehe: 09/07/2026

Dkt. Malenya Mary

TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa familia yangu kwa usaidizi wao hasa mama yangu Eunice, mwanangu Eunice, kaka zangu na dada zangu John, Nick, Vinah na Judy. Aidha kazi hii ninaitabaruku kwa walimu na wasomi wenzangu ambao wamenisaidia kwa safari yangu ya masomo.

SHUKRANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake, afya njema na uwezo alionipa hadi kukamilisha kazi hii. Aidha, ninamshukuru Mungu kwa ajili ya familia yangu kwa upendo, maombi na msaada wao usio na kikomo katika kipindi chote cha masomo yangu.

Ninatambua na kuthamini juhudi za walimu wangu walionilea kitaaluma kuanzia elimu ya msingi, sekondari hadi shahada ya kwanza. Kazi hii ni matokeo ya juhudi za pamoja, kujitolea na msaada wa watu mbalimbali walionisaidia katika hatua tofauti za safari yangu ya kielimu.

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wa utafiti huu, Dkt. Rose Mavisi, Mkuu wa Idara ya Lugha na Mawasiliano, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki (CUEA), na Dkt. Mary Malenya, kwa ukarimu, kujitolea na utaalamu wao. Walinipa mwongozo, ushauri na maoni muhimu yaliyosaidia kuboresha kazi hii. Vilevile, ninawashukuru wahadhiri wangu wote wa Idara, hususan Dkt. Rose Mavisi, Dkt. Lina Akaka, Bw. Bogonko na Bw. Morgan Adero, kwa kunielekeza na kunisaidia katika kozi zangu za uzamili. Mungu awabariki kwa juhudi na kujitolea kwao.

Ninawashukuru pia wanazuoni wenzangu, Remmy, Erick, Irene, Miriam, Perpetua na Sharon, kwa michango, ushirikiano na moyo wa kusaidiana katika kipindi chote cha masomo. Mchango wao ulikuwa muhimu katika safari hii ya kielimu.

Vilevile, ninatoa shukrani za pekee kwa familia yangu, hasa mama yangu mpendwa, Eunice; mwanangu, Eunice; kaka zangu, Nick na John; dada zangu, Vinah na Judy; pamoja na jamaa zangu wa karibu. Nawashukuru kwa upendo, moyo wa kunitia moyo, maombi na msaada wao katika kufanikisha masomo yangu.

Mwisho, ninawashukuru marafiki zangu wote ambao siwezi kuwataja kwa majina kwa sababu ya wingi wao, kwa maombi, ushauri, msaada na kunitia moyo katika kipindi chote cha utafiti na masomo yangu. Kwa ujumla, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa kila mmoja aliyetoa mchango wa aina yoyote katika kufanikisha utafiti huu. Mungu awabariki sana.

IKISIRI

Dini ni mojawapo ya taasisi muhimu za kijamii zinazoathiri maadili, mitazamo, mahusiano na mienendo ya watu katika jamii mbalimbali. Katika fasihi ya Kiswahili, dini imekuwa ikisawiriwa kwa namna mbalimbali kutokana na nafasi yake katika maisha ya jamii, ikiwamo kujenga maadili, kutoa matumaini na kuathiri mahusiano pamoja na mamlaka. Hata hivyo, tafiti nyingi zilizotangulia katika fasihi ya Kiswahili zimejikita zaidi katika masuala ya kijamii na kisiasa, huku zikitoa nafasi finyu kwa uchanganuzi wa kina wa namna matini zinavyojenga, kuvuruga na kubadilisha maana ya dini na uongozi wa kidini. Pengo hili la kifasihi ndilo lililoongoza utafiti huu. Utafiti ulilenga kuchanganua taswira ya dini katika riwaya teule, kubainisha athari za dini katika maadili ya jamii katika riwaya teule, na kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini katika riwaya teule. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Udenguzi iliyoasisiwa na Jacques Derrida na kuendelezwa na wanazuoni wengine, ambayo inasisitiza kuwa maana katika matini si thabiti bali inaweza kuvurugwa na kujengwa upya kulingana na muktadha. Mihimili mitatu ya nadharia hii ilitumika kuongoza uchanganuzi. Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo na ulilenga fasihi ya Kiswahili kama eneo la utafiti, huku riwaya ya *Paradiso* ikiteuliwa kimakusudi kama sampuli kwa sababu inabeba taswira pana na changamano za dini na viongozi wa dini. Data zilikusanywa kupitia usomaji wa kina wa riwaya teule zaidi ya mara moja, ambapo dondoo zinazohusiana na malengo ya utafiti zilitambuliwa, kunukuliwa na kuainishwa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kimaelezo kwa kuhusisha dondoo za matini na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi, huku ukizingatia mikinzano, maana zinazopingana na maana zilizofichika katika matini. Utafiti ulibaini kuwa taswira ya dini katika *Paradiso* ni pana na yenye sura zinazokinzana, ambapo dini inasawiriwa kama chanzo cha tumaini, wokovu na maendeleo, lakini wakati huo huo kama chombo cha migogoro, unyonyaji na ukandamizaji. Aidha, dini imebainika kuathiri maadili ya jamii kwa namna chanya na hasi. Kwa upande chanya, dini inahusishwa na kuimarisha umoja, uwajibikaji na mshikamano wa jamii, ilhali kwa upande hasi inahusishwa na chuki, unafiki, ubinafsi na migogoro. Viongozi wa dini wamesawiriwa kwa namna changamano, ambapo baadhi yao wanaonekana kuwa waaminifu na waadilifu, huku wengine wakidhihirisha udhaifu wa kibinadamu na matumizi mabaya ya mamlaka ya kidini. Kwa jumla, utafiti umebaini kuwa maana ya dini katika matini si thabiti, bali hubadilika kulingana na matendo ya wahusika, mazingira na muktadha wa matukio. Utafiti huu unapanua maarifa ya kifasihi kwa kuonyesha namna Nadharia ya Udenguzi inavyoweza kutumiwa katika uchanganuzi wa taswira ya dini katika riwaya ya Kiswahili. Inapendekezwa tafiti zaidi zichunguze taswira ya dini katika riwaya nyingine za Kiswahili, matumizi ya nadharia nyingine za uhakiki wa fasihi katika uchanganuzi wa dini, pamoja na usawiri wa viongozi wa dini katika kazi mbalimbali za fasihi.

ABSTRACT

Religion is one of the important social institutions that influences morals, attitudes, relationships and the behaviour of people in various societies. In Kiswahili literature, religion has been portrayed in different ways because of its role in social life, including shaping morals, providing hope and influencing relationships and authority. However, most previous studies in Kiswahili literature have focused more on social and political issues, while giving limited attention to in-depth analysis of how texts construct, destabilise and transform the meaning of religion and religious leadership. This literary gap guided the present study. The study aimed to analyse the portrayal of religion in the selected novel, establish the effects of religion on social morals in the selected novel, and analyse the portrayal of religious leaders in the selected novel. The study was guided by Deconstruction Theory, founded by Jacques Derrida and developed by other scholars, which emphasises that meaning in a text is not fixed but can be destabilised and reconstructed depending on context. Three tenets of the theory guided the analysis. The study adopted a descriptive design and focused on Kiswahili literature as the area of study, while the novel *Paradiso* was purposively selected as the sample because it contains broad and complex portrayals of religion and religious leaders. Data were collected through repeated close reading of the selected novel, whereby excerpts related to the study objectives were identified, extracted and organised. Data analysis was descriptive and involved relating textual excerpts to the tenets of Deconstruction Theory while focusing on contradictions, conflicting meanings and meanings concealed within the text. The study established that the portrayal of religion in *Paradiso* is broad and characterised by contradictory dimensions, with religion portrayed as a source of hope, salvation and progress, while at the same time functioning as a tool of conflict, exploitation and oppression. The study further established that religion affects social morals both positively and negatively. Positively, religion is associated with strengthening unity, accountability and social cohesion, while negatively, it is associated with hatred, hypocrisy, selfishness and conflict. Religious leaders are portrayed in complex ways, with some depicted as faithful and upright, while others exhibit human weaknesses and abuse of religious authority. Overall, the study established that the meaning of religion in the text is not fixed but changes according to the actions of characters, circumstances and the context of events. The study expands literary knowledge by demonstrating how Deconstruction Theory can be applied in analysing the portrayal of religion in the Kiswahili novel. It recommends further studies on the portrayal of religion in other Kiswahili novels, the application of other literary theories in analysing religion, and the portrayal of religious leaders in different literary works.

.

ISTILAHI MAALUMU

Dini: Mfumo wa imani, ibada, maadili na mitazamo unaohusisha uhusiano wa binadamu na masuala ya kiroho na unaoweza kuathiri maisha ya mtu na jamii. Katika utafiti huu, dini inachunguzwa kama kipengele cha kifasihi kinachojengwa na matini kupitia wahusika, matukio, imani, taasisi na matendo.

Taswira ya dini: Namna dini inavyowasilishwa, kujengwa na kupewa maana katika matini ya kifasihi. Katika utafiti huu, istilahi hii inahusu sura mbalimbali za dini zinazojitokeza katika Paradiso, zikiwamo taswira chanya na hasi pamoja na maana zinazokinzana.

Viongozi wa dini: Watu wanaopewa mamlaka au nafasi ya kuongoza shughuli za kidini, kutoa mwongozo wa kiroho na kimaadili na kuwaelekeza waumini. Katika utafiti huu, istilahi hii inahusu wahusika wanaotekeleza au kuhusishwa na nafasi za uongozi wa kidini katika Paradiso.

Usawiri wa viongozi wa dini: Namna mwandishi anavyowajenga na kuwawasilisha viongozi wa dini kupitia sifa, kauli, matendo, mahusiano na nafasi zao katika matini. Utafiti huu unazingatia pia mikinzano kati ya matarajio ya jamii kuhusu viongozi wa dini na matendo yao.

Maadili ya jamii: Misingi, kanuni, thamani na mienendo inayotumiwa na jamii kutofautisha mwenendo unaokubalika na usiokubalika. Katika utafiti huu, maadili yanahusishwa na namna dini inavyochangia kujenga, kuimarisha au kudhoofisha umoja, kusaidiana, msamaha, uwajibikaji na mwenendo wa wanajamii.

Athari za dini katika maadili ya jamii: Mabadiliko au matokeo yanayohusishwa na dini katika mienendo na mahusiano ya wanajamii. Katika utafiti huu, athari hizo zinachunguzwa kwa kuzingatia pande chanya na hasi zinazojitokeza katika Paradiso.

Nadharia ya Udenguzi: Mkabala wa uhakiki unaochunguza kutokuwa thabiti kwa maana, mikinzano ya ndani ya matini na uwezekano wa matini kujenga na wakati huohuo kupinga au kujibomoa yenyewe. Katika utafiti huu, Nadharia ya Udenguzi inatumika kuchanganua taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

Uchanganuzi wa kifasihi: Mchakato wa kuchunguza vipengele vya matini kwa kina ili kubaini namna vinavyojengwa, vinavyohusiana na vinavyozalisha maana. Katika utafiti huu, uchanganuzi unafanywa kwa kuongozwa na Nadharia ya Udenguzi.

Mkabala wa kithamano: Mkabala wa utafiti unaojikita katika data za maneno, maana, muktadha na tafsiri badala ya kutegemea vipimo vya kitakwimu. Utafiti huu unatumia mkabala huu kwa sababu data yake kuu inatokana na matini ya kifasihi.

AKRONIMU NA VIFUPISHO

CUEA: Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki (The Catholic University of Eastern Africa)

NACOSTI: Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (National Commission for Science, Technology and Innovation)

U.K: Ukurasa

YALIYOMO

UNGAMO ..... **ii**

TABARUKU ..... **iii**

SHUKRANI ..... **iv**

IKISIRI ..... **v**

ABSTRACT ..... **vi**

ISTILAHI MAALUMU ..... **vii**

AKRONIMU NA VIFUPISHO ..... **ix**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI **1**

1.0 Utangulizi 1

1.1 Usuli wa Mada 1

1.1.1 Historia ya Dini 2

1.2 Tatizo la Utafiti 3

1.3 Malengo ya Utafiti 4

1.4 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Sababu za Kuchagua Mada 5

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti 5

MAPITIO YA MAANDISHI **6**

2.1 Utangulizi 6

2.2 Mapitio ya maandishi 6

2.2.1 Taswira ya Dini katika Fasihi 6

2.2.2 Athari ya Dini katika Maadili ya Kijamii 10

2.2.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii 17

SURA YA TATU **31**

MBINU ZA UTAFITI..... 31
3.0 Utangulizi..... 31
3.1 Muundo wa Utafiti..... 31
3.2 Eneo la Utafiti..... 32
3.3 Kundi Lengwa..... 32
3.4 Sampuli na Usampulishaji..... 33
3.5 Ukusanyaji Data..... 33
3.6 Uchanganuzi wa data..... 34
3.7 Uthabiti wa data..... 34
3.7.1 Usahihi wa data..... 35
3.7.2 Kuaminika kwa data za utafiti..... 35
3.8 Maadili ya Utafiti..... 36
3.9 Hitimisho la Sura ya Tatu..... 37
SURA YA NNE..... 38
UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA..... 38
4.0 Utangulizi..... 38
4.1 Taswira ya Dini katika Riwaya ya *Paradiso*..... 38
4.1.1 Dini kama Chanzo cha Tumaini..... 39
4.1.2 Dini kama Njia ya Wokovu..... 40
4.1.3 Dini kama Chanzo cha Miujiza na Uponyaji..... 40
4.1.4 Dini kama Wito wa Mtu..... 41
4.1.5 Dini kama Chanzo cha Migogoro na Utengano..... 42
4.1.6 Dini kama Mfumo Wenye Kanuni Kali..... 42
4.1.7 Dini kama Chombo cha Unyanyasaji na Unyonyaji..... 43
4.1.8 Dini kama Chanzo cha Maendeleo katika Jamii..... 44

4.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini katika Riwaya ya *Paradiso* 44
4.2.1 Viongozi wa Dini kama Waaminifu 45
4.2.2 Viongozi wa Dini kama Waadilifu 45
4.2.3 Viongozi wa Dini kama Wavumilivu 46
4.2.4 Viongozi wa Dini kama Wenye Bidii 47
4.2.5 Viongozi wa Dini kama Wawajibikaji 47
4.2.6 Viongozi wa Dini kama Wenye Tamaa na Ubinafsi 48
4.2.7 Viongozi wa Dini kama Wanafiki 48
4.2.8 Viongozi wa Dini kama Wenye Nguvu za Miujiza 49
4.2.9 Viongozi wa Dini kama Washauri na Waelekezi 50
4.2.10 Viongozi wa Dini kama Wenye Udhaifu wa Kibinadamu 50
4.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii katika Riwaya ya *Paradiso* 51
4.3.1 Athari Chanya 51
4.3.1.1 Dini Imeleta Umoja Baina ya Wanajamii 52
4.3.1.2 Dini Imepunguza Vitendo Viovu katika Jamii 52
4.3.1.3 Dini Imehimiza Kusaidiana kati ya Watu 53
4.3.1.4 Dini Imeimarisha Msamaha kati ya Watu 53
4.3.1.5 Dini Imekuza Uwajibikaji Miongoni mwa Watu 54
4.3.2 Athari Hasi 54
4.3.2.1 Dini Imeleta Migogoro na Migawanyiko 54
4.3.2.2 Dini Imesababisha Chuki Baina ya Waumini 55
4.3.2.3 Dini Imechochea Tamaa na Ubinafsi Miongoni mwa Viongozi 56
4.3.2.4 Dini Imechochea Msimamo Mkali 56
4.3.2.5 Dini Imechangia Unafiki Miongoni mwa Waumini 57
4.4 Hitimisho 57

SURA YA TANO 59
5.1 Utangulizi 59
5.2 Muhtasari wa Tasnifu 59
5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 60
5.3.1 Taswira ya Dini katika Riwaya Teule 60
5.3.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini katika Riwaya Teule 60
5.3.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii katika Riwaya Teule 60
5.4 Hitimisho 61
5.4.1 Taswira ya Dini 61
5.4.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini 61
5.4.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii 61
5.4.4 Mchango wa Nadharia ya Udenguzi 62
5.5 Mapendekezo ya Utafiti 62
5.5.1 Mapendekezo ya Kijumla 62
5.5.2 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye 62
MAREJELEO 64
VIAMBATISHO 68
KIAMBATISHO I: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki 68
KIAMBATISHO II: Kibali cha NACOSTI 69
KIAMBATISHO III: FOMU YA UCHANGANUZI WA DATA 70

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza msingi na mwelekeo wa utafiti kuhusu uchanganuzi wa taswira ya dini katika riwaya ya *Paradiso* ya John Habwe. Inajumuisha usuli wa mada, historia ya dini, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya utafiti. Sehemu hizi zimewasilishwa kwa mtiririko unaoelekeza katika kuelewa suala linalochunguzwa na pengo la kifasihi linalokusudiwa kushughulikiwa na utafiti huu.

1.1 Usuli wa Mada

Dini ni mojawapo ya masuala yanayojitokeza katika maisha ya binadamu na jamii. Dini huhusisha imani, maadili, ibada na mitazamo kuhusu maisha na ulimwengu. Durkheim (1912) anaeleza dini kama mfumo wa imani na desturi unaowaunganisha watu katika jamii. Kwa mtazamo wa Freud (1927), dini inahusishwa na mahitaji na hofu za kisaikolojia za binadamu, ilhali Marx (1844) anaiona dini kama mfumo unaoweza kutoa faraja kwa watu wanaokabiliwa na mateso ya kijamii na kiuchumi. Mitazamo hii inaonyesha kuwa dini inaweza kutazamwa kwa namna tofauti kulingana na mazingira na mtazamo wa mtafiti.

Mbiti (1969) anaeleza kuwa dini imefungamana kwa karibu na maisha ya Mwafrika. Kwa mtazamo huu, dini haiwezi kutenganishwa na masuala ya kijamii, kitamaduni na kimaadili. Hivyo, dini inaweza kuwa chanzo cha mshikamano na maadili, lakini pia inaweza kuhusishwa na migongano inayotokana na namna inavyotumiwa na wanajamii. Mazrui na Shariff (1994) wanaonyesha kuwa dini katika mazingira ya Kiafrika inaweza kuwasilishwa kama nguzo ya maadili au kama chombo cha kuathiri fikra na maisha ya jamii.

Uhusiano kati ya dini na fasihi ni muhimu kwa sababu fasihi huakisi na kuchunguza masuala yanayohusu maisha ya jamii. Waandishi wa fasihi wanaweza kutumia wahusika, matukio, lugha na dhamira mbalimbali kuonyesha namna dini inavyoeleweka na kutumiwa katika jamii. Wamitila (2002) anaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili imekuwa ikitumia dini kuonyesha mgongano kati ya maadili yanayohusishwa na dini na namna dini inavyoweza kutumiwa kwa manufaa binafsi. Hali

hii huweza kujitokeza kupitia wahusika wanaotumia dini kuficha au kuhalalisha matendo yao. Kwa hiyo, dini katika fasihi haiwasilishwi kwa taswira moja isiyobadilika, bali inaweza kuonekana kwa mitazamo inayokinzana.

Katika riwaya ya Kiswahili, dini inaweza kujitokeza kupitia imani, ibada, taasisi za kidini, viongozi wa dini na athari zake katika maisha ya jamii. Uwasilishaji wa vipengele hivi unaweza kuibua taswira tofauti za dini, ikiwemo dini kama chanzo cha maadili na faraja, lakini pia kama mfumo unaoweza kutumiwa vibaya na baadhi ya wahusika. Mtazamo huu unafanya dini kuwa suala muhimu la kifasihi linalohitaji kuchanganuliwa kwa kuzingatia namna linavyojengwa na matini.

Katika *Paradiso*, Habwe (2005) anawasilisha masuala yanayohusiana na dini na maisha ya jamii. Riwaya hii inatoa nafasi ya kuchunguza namna dini inavyosawiriwa, namna viongozi wa dini wanavyowasilishwa na namna dini inavyohusishwa na maadili ya jamii. Kwa kuzingatia kwamba matini inaweza kuwa na mitazamo na maana zinazokinzana, kuna haja ya kuichanganua *Paradiso* kwa kuangalia namna taswira ya dini inavyojengwa na pia namna inavyoweza kujitengua ndani ya matini yenyewe. Utafiti huu, kwa hiyo, unajikita katika uchanganuzi wa kifasihi wa taswira ya dini katika *Paradiso* kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi.

1.1.1 Historia ya Dini

Dini imekuwa sehemu ya maisha ya jamii tangu nyakati za kale. Durkheim (1912) anaiona dini kama mfumo wa imani, ibada na maadili unaowaunganisha wanajamii. Katika jamii za kale, dini ilihusishwa pia na utawala na maisha ya kijamii. Eliade (1957) anaonyesha uhusiano kati ya dini na mifumo ya maisha ya jamii za kale, ambapo mamlaka ya kisiasa na imani za kidini ziliweza kuhusiana kwa karibu. Baadaye, mitazamo kuhusu dini ilibadilika kadiri jamii na fikra za binadamu zilivyobadilika.

Katika mazingira ya Afrika, Mbiti (1969) anaonyesha kuwa dini za jadi zilifungamana na maisha ya kila siku ya jamii. Imani, mila na uhusiano na mababu vilikuwa sehemu ya mfumo wa maisha ya jamii. Pamoja na hayo, ujio wa dini za kigeni, hasa Ukristo na Uislamu, ulibadilisha kwa kiasi kikubwa mazingira ya kidini barani Afrika. Mudimbe (1988) anaonyesha kwamba ukoloni uliambatana na mabadiliko ya fikra na mifumo ya maisha ya Waafrika, jambo lililoathiri pia namna dini za Kiafrika zilivyotazamwa.

Katika Afrika Mashariki, dini ya Uislamu ilienea hasa katika maeneo ya pwani, huku Ukristo ukienea zaidi katika maeneo mbalimbali ya bara wakati wa ukoloni. Dini hizi ziliathiri maisha ya jamii katika maeneo kama elimu, utamaduni na maadili. Mazrui na Shariff (1994) wanaonyesha kuwa dini katika fasihi ya Kiafrika imeweza kuwasilishwa kwa mitazamo tofauti, ikiwa ni pamoja na kama msingi wa maadili na kama mfumo unaoweza kuhusishwa na mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni.

Historia hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inasaidia kuelewa mazingira ambayo ndani yake dini imejengwa na kupewa maana katika jamii. Hata hivyo, utafiti huu hauchunguzi historia ya dini kwa upana, bali unatumia historia hiyo kama msingi wa kuelewa namna dini inavyowasilishwa katika fasihi ya Kiswahili, hususan katika *Paradiso*. Baadhi ya mitazamo kuhusu dini kama mfumo wa maadili, mamlaka na taasisi ya kijamii itatumika pia katika uchanganuzi wa matini katika Sura ya Nne.

1.2 Tatizo la Utafiti

Dini ni suala muhimu katika maisha ya jamii na pia ni mojawapo ya masuala yanayowasilishwa katika fasihi ya Kiswahili. Waandishi wa fasihi wameendelea kutumia dini kuwasilisha imani, maadili, migogoro ya kijamii na mahusiano ya mamlaka. Hata hivyo, namna dini inavyowasilishwa katika kazi ya fasihi inaweza kuwa na mitazamo inayokinzana. Dini inaweza kuonekana kama chanzo cha maadili na mwongozo wa jamii, lakini wakati huo huo matendo ya baadhi ya wahusika yanaweza kuonyesha matumizi ya dini kwa manufaa binafsi au namna taasisi za dini zinavyoweza kukengeuka kutoka katika matarajio ya jamii.

Tafiti zilizotangulia kuhusu dini katika fasihi zimeangazia vipengele mbalimbali vya dini na uhusiano wake na jamii. Hata hivyo, bado kuna haja ya kuchunguza kwa kina namna taswira ya dini inavyojengwa na kujitokeza kwa maana zinazokinzana ndani ya matini ya kifasihi. Pengo hili ni la kifasihi kwa sababu linahusu namna mwandishi anavyowasilisha dini kupitia matini, wahusika, matendo na mahusiano yao, badala ya kuchunguza dini kama suala la kitheolojia au kijamii pekee.

Katika *Paradiso*, Habwe (2005) anawasilisha masuala yanayohusiana na dini, viongozi wa dini na maadili ya jamii. Hata hivyo, kuna haja ya kuchanganua namna vipengele hivyo vinavyounda taswira ya dini na namna maana zinazohusishwa na dini zinavyoweza kukinzana ndani ya matini.

Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu linatokana na haja ya kuziba pengo la kifasihi katika uchanganuzi wa taswira ya dini katika *Paradiso* kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi. Utafiti huu unalenga kuchanganua taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii kama vinavyojitokeza katika riwaya teule.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kuchanganua taswira ya dini katika riwaya teule.
2. Kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini katika riwaya teule.
3. Kubainisha athari za dini katika maadili ya jamii katika riwaya teule.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Taswira ya dini imejitokezaje katika riwaya teule?
2. Viongozi wa dini wamesawiriwaje katika riwaya teule?
3. Dini ina athari gani katika maadili ya jamii katika riwaya teule?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu wa kitaaluma na kifasihi kwa sababu unachangia katika kukuza uelewa wa namna dini inavyowasilishwa katika fasihi ya Kiswahili. Kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi, utafiti unaonyesha namna matini ya kifasihi inavyoweza kujenga taswira mbalimbali za dini na pia kuibua maana zinazokinzana kuhusu dini, viongozi wake na nafasi yake katika maadili ya jamii. Kwa msingi huu, utafiti unatoa mchango katika mijadala ya kitaaluma kuhusu uhusiano kati ya dini na fasihi ya Kiswahili.

Utafiti huu unaweza kuwa na manufaa kwa watafiti na wasomi wa fasihi ya Kiswahili kwa kuwapa msingi wa kuendeleza tafiti kuhusu dini katika kazi nyingine za kifasihi. Pia, utafiti unaweza kuwasaidia wanafunzi na walimu wa fasihi kuelewa namna suala la dini linavyoweza kuchanganuliwa katika matini ya kifasihi kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi.

Aidha, utafiti huu unaweza kuwa na manufaa kwa wasomaji wa fasihi kwa kuwa unawawezesha kutambua mitazamo mbalimbali kuhusu dini kama inavyowasilishwa katika *Paradiso*. Kwa

kufanya hivyo, utafiti unaonyesha umuhimu wa kuisoma kazi ya fasihi kwa mtazamo unaozingatia uwepo wa maana nyingi na zinazoweza kukinzana ndani ya matini.

1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii ilichaguliwa kutokana na umuhimu wa dini kama mojawapo ya masuala yanayojitokeza katika fasihi ya Kiswahili na maisha ya jamii. Utafiti kuhusu taswira ya dini katika *Paradiso* unatoa fursa ya kuchunguza namna dini inavyowasilishwa katika matini ya kifasihi na namna taswira hiyo inavyoweza kuwa na mitazamo mbalimbali na inayokinzana. Aidha, mada hii ilichaguliwa kwa sababu kuna haja ya kuendeleza uchanganuzi wa kifasihi kuhusu dini kwa kutumia mitazamo ya kinadharia inayoweza kufichua maana zinazojitokeza ndani ya matini. Utafiti huu pia unatarajiwa kuwa rejeleo kwa watafiti watakaoshughulikia masuala ya dini katika kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili.

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika uchanganuzi wa taswira ya dini katika riwaya ya *Paradiso* ya John Habwe (2005). Utafiti umejikita katika vipengele vitatu vinavyoendana na malengo yake: taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii. Utafiti umetumia Nadharia ya Udenguzi kama msingi wa kuchanganua namna maana kuhusu dini zinavyojengwa, zinavyokinzana na zinavyoweza kujitengua ndani ya matini.

Paradiso iliteuliwa kimakusudi kwa sababu inatoa matukio na wahusika wanaowezesha kuchunguza vipengele vya dini vinavyolengwa na utafiti huu. Utafiti umejikita katika matini ya riwaya yenyewe na haukulenga kuchanganua dini kwa mtazamo wa kitheolojia au kijamii kwa ujumla. Vilevile, haukulenga kuchanganua riwaya nyingine za Habwe au kazi nyingine za kifasihi ambazo hazikuteuliwa katika utafiti huu. Mipaka hii iliwekwa ili utafiti ubaki katika lengo lake kuu la kuchanganua taswira ya dini katika *Paradiso* kwa mtazamo wa kifasihi na kinadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alipitia kazi zilizoandikwa awali kuhusu uchanganuzi wa taswira ya dini. Kazi hizi zilijumuisha tasnifu, vitabu, majarida na tafiti za fasihi kuhusu uchanganuzi wa taswira ya dini zilizofanywa na watafiti mbalimbali. Mapitio ya kazi hizi yameonyesha pengo lililopelekea utafiti huu kufanywa na mchango ambao umetoa kiakademia kudhihirika. Sura hii pia imefafanua nadharia iliyotumiwa kuchanganua data ya utafiti huu.

2.2 Mapitio ya maandishi

Sehemu hii inahusu mapitio ya maandishi ya kitaaluma yanayohusiana na mada ya utafiti huu. Mapitio yamefanywa kwa kuzingatia tafiti na maandiko yanayohusu dini, usawiri wa viongozi wa dini pamoja na uhusiano kati ya dini na maadili ya jamii katika fasihi. Lengo la mapitio haya ni kubainisha maarifa yaliyopo kuhusu masuala yanayochunguzwa, kuonyesha mitazamo na matokeo ya watafiti mbalimbali, na hatimaye kubainisha pengo ambalo utafiti huu unalenga kuliziba.

2.2.1 Taswira ya Dini katika Fasihi

Dini ni mojawapo ya masuala yanayojitokeza katika kazi za fasihi kwa kuwa inahusiana na imani, maadili, mienendo na mahusiano ya wanajamii. Katika fasihi, dini inaweza kusawiriwa kama chanzo cha matumaini, mshikamano na mwongozo wa kimaadili, lakini pia inaweza kuwasilishwa kama taasisi yenye migongano, dhuluma, unafiki, tamaa ya mali na matumizi mabaya ya mamlaka. Kwa msingi huu, taswira ya dini haiwezi kuchukuliwa kuwa na maana moja isiyobadilika, bali hujengwa kupitia mitazamo na matendo mbalimbali yanayoweza kukinzana. Mapitio katika sehemu hii yanazingatia tafiti zilizochunguza namna dini inavyowasilishwa katika fasihi na katika miktadha inayohusiana na fasihi. Tafiti zimepangwa kwa mtiririko wa miaka ili kuonyesha maendeleo ya mjadala na kubainisha eneo ambalo bado halijashughulikiwa kikamilifu.

Karanja (2005), katika tasnifu yake, alichunguza nafasi ya dini katika jamii ya kisasa kama inavyosawiriwa katika riwaya *Nguvu ya Sala*, *Walenisi* na *Babu Alipofufuka*. Karanja alibaini kuwa dini katika jamii ya kisasa imepoteza kwa kiasi fulani nafasi yake muhimu ya awali, hali inayowafanya wanajamii kuhitajika kuchunguza na kutofautisha mema na mabaya yanayojitokeza

katika imani za kidini. Aidha, alionyesha kuwa baadhi ya watu wameidunisha dini kiasi cha kujiona kama miungu ya kuabudiwa, huku wengine wakipoteza imani kutokana na kushindwa kwa dini kutoa suluhisho la matatizo yao ya kimaisha. Kwa hiyo, utafiti wa Karanja unaonyesha taswira kinzani ya dini, ambapo dini inayotarajiwa kuwa chanzo cha mwongozo na tumaini inaweza pia kuhusishwa na kukatishwa tamaa kwa waumini. Hata hivyo, Karanja alijikita katika nafasi ya dini katika jamii ya kisasa kwa kurejelea riwaya tatu, ilhali utafiti huu unalenga kuchanganua kwa kina taswira ya dini katika riwaya moja ya *Paradiso* kwa mtazamo wa Udenguzi.

Ng'etich (2011), katika tasnifu yake ya uzamili, alichunguza dini kama chombo cha kuwadhulumu waumini katika *Paradiso*, *Nguvu ya Sala*, *Nitaolewa Nikipenda* na *Masaibu ya Ndugu Jero*. Matokeo yake yalionyesha kuwa dini inaweza kuhusishwa na aina mbalimbali za dhuluma, zikiwamo za kihisia, kimwili, kiuchumi, kifamilia na kiakili. Alibainisha pia kuwa tamaa, ubinafsi, umaskini, kutoelewa mafundisho ya dini na kuwategemea viongozi dhalimu ni miongoni mwa mambo yanayoweza kuchangia dhuluma za kidini. Hoja hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inafichua mvutano kati ya matarajio ya dini kuwa kimbilio la mwanadamu na namna inavyoweza kugeuka chanzo cha dhuluma. Hata hivyo, msisitizo wa Ng'etich ulikuwa katika dhuluma dhidi ya waumini, wakati utafiti huu unaangazia kwa upana zaidi taswira ya dini, ikiwamo namna taasisi ya dini inavyojengwa kupitia matendo, imani na mahusiano mbalimbali katika *Paradiso*.

Jesse, King'ei na Wafula (2019) walijadili matumizi ya dini katika mazingira ya utandawazi na namna dini inavyoweza kuhusishwa na mifumo ya kiuchumi na kiutawala. Kwa mujibu wa mjadala wao, utandawazi unaweza kuchangia hali ambapo mataifa yenye nguvu kiuchumi yanaendelea kuhifadhi utajiri na maslahi yao huku watu katika mataifa yanayoendelea wakizidi kutegemea dini kama chanzo cha suluhisho. Hali hiyo inaweza kuzalisha kukatishwa tamaa kwa waumini pale matarajio yao ya kidini yanapokinzana na hali halisi ya maisha. Utafiti huu unatoa mtazamo mpana wa kuelewa namna dini inavyoweza kuhusishwa na masuala ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, haukulenga uchanganuzi wa matini ya riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu, kwa upande wake, unachanganua namna mahusiano hayo yanavyojengwa kisanaa ndani ya *Paradiso*, hivyo kuhamisha mjadala kutoka katika mazingira ya kijamii kwa jumla hadi katika usawiri wa dini ndani ya matini ya kifasihi.

Princewell (2017) anaiona dini kama mfumo unaoweza kugeuzwa kuwa biashara, ambapo imani ya waumini inaweza kutumiwa kama mtaji wa kujipatia manufaa. Mtazamo huu unaonyesha

mabadiliko ya taswira ya dini kutoka taasisi inayotarajiwa kujikita katika masuala ya kiroho na maadili hadi taasisi inayoweza kuhusishwa na maslahi ya kiuchumi. Kwa hivyo, hoja ya Mhango inasaidia kufafanua upande mmoja wa taswira kinzani ya dini, yaani hali ambapo kile kinachotarajiwa kuwa kitakatifu kinaweza kuhusishwa na shughuli za kibiashara. Hata hivyo, mjadala wake unatokana na uchapisho wa jarida na haujajikita katika uchanganuzi wa riwaya ya Kiswahili. Utafiti huu unachunguza jinsi hali hiyo inavyowasilishwa na kujengwa kupitia wahusika, matukio na mahusiano katika *Paradiso*.. Alichunguza pia ugeuzaji wa dini kuwa biashara nchini Nigeria na kubainisha kuwa dini imepoteza sehemu ya nafasi yake ya awali ya kuwa taasisi takatifu na mjenzi wa tabia na maadili ya jamii. Kwa mujibu wa utafiti huo, ongezeko la makanisa na msisitizo wa utajiri na mafanikio ya haraka vimechangia kuibuka kwa matumizi mabaya ya dini. Baadhi ya viongozi hutumia upotoshaji wa mafundisho, vitisho, ulaghai na mbinu nyingine kuwashawishi waumini kutoa fedha. Matokeo haya yanaonyesha kuwa taswira ya dini inaweza kujengwa kupitia mvutano kati ya wajibu unaotarajiwa wa dini na matendo yanayotekelezwa na baadhi ya wahusika wake. Ingawa utafiti wa Princewell una mchango katika kuelewa taswira ya dini inayohusishwa na biashara na ulaghai, ulijikita katika mazingira ya Nigeria na haukuchanganua matini ya kifasihi. Utafiti huu unapanua mjadala huo kwa kuchunguza namna taswira hiyo inavyojengwa ndani ya riwaya ya Kiswahili *Paradiso*.

Ikunga na Abiobio (2018) walichunguza changamoto zinazolikabili Kanisa nchini Nigeria na kubainisha kuwa badala ya kujikita katika malezi ya kiroho, baadhi ya taasisi za kidini zimeelekea katika kujilimbikizia mali na kuhusisha shughuli za kanisa na siasa. Walionyesha pia kuwa baadhi ya viongozi wa dini hujihusisha na kampeni za kisiasa na kujenga uhusiano na wanasiasa kwa matarajio ya kupata manufaa ya kifedha. Hali hii inazua kinaya kati ya jukumu linalotarajiwa la dini na matendo yanayotekelezwa na taasisi na viongozi wake. Utafiti wao kwa hiyo una umuhimu katika kuelewa taswira ya dini kama taasisi inayoweza kuathiriwa na maslahi ya kiuchumi na kisiasa. Hata hivyo, utafiti huo haukuchanganua jinsi kinaya hicho kinavyoundwa kisanaa katika kazi ya fasihi ya Kiswahili. Pengo hilo linaifanya *Paradiso* kuwa eneo muhimu la kuchunguza namna maana za dini zinavyojengwa na wakati huohuo kupingwa ndani ya matini.

Oko na Umanah (2022) walichunguza ongezeko la makanisa nchini Nigeria na athari zake katika maendeleo ya kitaifa. Walibaini kuwa ongezeko hilo limeambatana na matatizo mbalimbali, miongoni mwao ikiwa ni kuibuka kwa viongozi wanaoanzisha makanisa kwa kuzingatia manufaa

ya kifedha badala ya wito wa kiroho. Baadhi yao huwatumia waumini kama chanzo cha fedha kwa ajili ya kujinunulia mali za kifahari. Matokeo haya yanaendeleza mjadala kuhusu mabadiliko ya taswira ya dini kutoka taasisi inayotarajiwa kutoa faraja na mwongozo hadi taasisi inayoweza kuhusishwa na unyonyaji wa waumini. Hata hivyo, Oko na Umanah walijikita katika maendeleo ya kitaifa na mazingira ya Nigeria, na hivyo hawakuchanganua namna taswira hii inavyojengwa katika matini ya kifasihi ya Kiswahili. Utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchanganua taswira ya dini kama inavyowasilishwa katika *Paradiso*.

Muli (2024) alichunguza athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana kwa kulinganisha *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*. Utafiti wake ulibaini kuwa baadhi ya vijana hukatishwa tamaa na dini kutokana na migogoro ya madhehebu, matumizi mabaya ya matoleo ya waumini, umiliki wa taasisi za kidini kama mali za familia na matumizi mabaya ya madaraka ya viongozi wa dini. Aidha, alibainisha kuwa baadhi ya viongozi walihusishwa na rushwa na matumizi ya nafasi za kidini kwa manufaa binafsi. Matokeo haya ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu yanaonyesha kuwa *Paradiso* tayari imejadiliwa katika muktadha wa migogoro na kinaya kinachohusiana na dini. Hata hivyo, Muli alijikita zaidi katika udhanaishi wa kidini na athari zake kwa vijana, ilhali utafiti huu unalenga kuchanganua taswira ya dini yenyewe na namna maana mbalimbali zinazohusiana nayo zinavyojitokeza na kukinzana katika riwaya hiyo.

Kwa jumla, tafiti zilizopitiwa zinaonyesha kuwa dini imesawiriwa kwa mitazamo mbalimbali na wakati mwingine kinzani. Karanja (2005) na Ng'etich (2011) wameonyesha, kupitia riwaya za Kiswahili, kuwa dini inaweza kuhusishwa na kupotea kwa imani, dhuluma na kukatishwa tamaa. Jesse, Wafula na King'ei (2011), Princewell (2017), Ikunga na Abiobio (2018) pamoja na Oko na Umanah (2022) wameendeleza mjadala kwa kuonyesha namna dini inavyoweza kuhusishwa na maslahi ya kiuchumi, kisiasa na kibiashara. Muli (2024), kwa upande wake, ameleta mjadala huo karibu zaidi na *Paradiso* kwa kuonyesha migogoro na matumizi mabaya ya dini yanayoweza kuwatamausha waumini.

Hata hivyo, mapitio haya yanaonyesha pengo muhimu. Tafiti nyingi zimejikita katika kipengele kimoja cha dini, kama vile dhuluma, biashara, udhanaishi au maendeleo ya taasisi za kidini. Aidha, baadhi ya tafiti zimejikita katika mazingira ya kijamii badala ya kuchanganua kwa kina jinsi matini ya kifasihi yenyewe inavyojenga taswira mbalimbali za dini. Hata pale *Paradiso* imechunguzwa, mkazo umewekwa zaidi katika dhuluma au udhanaishi kuliko kuchanganua kwa mtazamo wa

Udenguzi namna dini inavyowasilishwa kupitia maana zinazokinzana, zinazoingiliana na zinazoweza kujibomoa ndani ya matini. Kwa hiyo, utafiti huu unalenga kuziba pengo hilo kwa kuchanganua taswira ya dini katika riwaya *Paradiso* kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi.

2.2.2 Athari ya Dini katika Maadili ya Kijamii

Viongozi wa dini hupewa nafasi muhimu katika kazi za fasihi kwa sababu wanawakilisha taasisi za kidini na matarajio ya jamii kuhusu uongozi wa kiroho na kimaadili. Kwa kawaida, viongozi hawa hutarajiwa kuwa vielelezo vya maadili, waelekezi wa waumini, watetezi wa haki na wasuluhishi wa migogoro katika jamii. Hata hivyo, fasihi imewasawiri viongozi wa dini kwa mitazamo mbalimbali, ikiwamo kama waadilifu na wahudumu wa jamii, lakini pia kama wanafiki, walaghai, watafuta mali na madaraka, au washirika wa mifumo dhalimu. Mapitio katika sehemu hii yanaangazia tafiti zilizoshughulikia usawiri na nafasi ya viongozi wa dini, hasa katika kazi za fasihi, pamoja na tafiti za kijamii zinazosaidia kuelewa matarajio na changamoto zinazohusishwa na uongozi wa kidini. Tafiti zimepangwa kwa mtiririko wa miaka ili kuonyesha namna mjadala huu ulivyoendelea.

Ng'etich (2011), katika tasnifu yake ya uzamili, alichunguza dini kama chombo cha kuwadhulumu waumini katika riwaya *Paradiso*, *Nguvu ya Sala*, na tamthilia *Nitaolewa Nikipenda* na *Masaibu ya Ndugu Jero*. Miongoni mwa mambo aliyobaini ni kwamba baadhi ya viongozi wa dini hutumia nafasi zao kuwadhulumu waumini kisaikolojia, kimwili, kiuchumi, kifamilia na kiakili. Alibainisha pia mbinu mbalimbali zinazotumiwa na viongozi hao, zikiwamo kujifanya kuwa na ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu, kutoa ahadi zisizotimia, kutumia vitisho, kuhusisha umaskini na dhambi, kutumia maombi kuhalalisha matakwa ya watu wenye nguvu, pamoja na unafiki na kujiona kuwa karibu zaidi na Mungu kuliko waumini wengine. Aidha, alionyesha namna baadhi ya viongozi wanavyotumia mamlaka ya kidini kuwanyamazisha waumini na kuzuia uwezo wao wa kuhoji.

Utafiti wa Ng'etich ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu unaonyesha kuwa usawiri wa kiongozi wa dini unaweza kujengwa kupitia mvutano kati ya mamlaka anayodhaniwa kuwa nayo na matumizi halisi ya mamlaka hayo. Hata hivyo, ingawa Ng'etich alirejelea *Paradiso,* alichunguza kwa upana zaidi dhuluma za kidini katika kazi kadhaa na kutumia Nadharia ya Udenguzi pamoja na Nadharia ya Maadili. Utafiti huu, kwa upande mwingine, unalenga kuchanganua moja kwa moja usawiri wa viongozi wa dini katika *Paradiso* kama mojawapo ya vipengele vya taswira ya

dini kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi pekee. Hivyo, utafiti huu unapata nafasi ya kuendeleza mjadala wa Ng'etich kwa kuangalia si tu dhuluma zinazofanywa na viongozi, bali pia mikinzano inayojitokeza katika namna wanavyowasilishwa katika matini.

Mosha (2013), katika tasnifu yake ya uzamili, alichunguza usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi. Utafiti wake ulionyesha kuwa Padri amesawiriwa kama kiongozi wa kanisa mwenye jukumu la malezi ya kiroho na uendeshaji wa ibada. Pamoja na hayo, Padri pia amewasilishwa kama mwanadamu wa kawaida mwenye udhaifu na anayehusika katika matendo kama vile uzinzi, ulevi na ugomvi. Vilevile, mhusika huyo anaonekana kuwa mwelekezi na mwenye sauti na ushawishi katika jamii. Matokeo haya yanaonyesha kuwa kiongozi wa dini katika fasihi anaweza kupewa sifa mbili zinazokinzana, yaani kuwa mwakilishi wa utakatifu kwa upande mmoja na mwanadamu mwenye udhaifu kwa upande mwingine.

Mosha anatoa msingi muhimu wa kuchanganua ujenzi wa mhusika kiongozi wa dini katika fasihi. Hata hivyo, utafiti wake ulijikita katika mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi, ilhali utafiti huu unahusu viongozi wa dini mbalimbali kama wanavyosawiriwa katika *Paradiso*. Tofauti hii ni muhimu kwa sababu inapanua uchanganuzi kutoka kwa mhusika mmoja wa kidini hadi katika namna nafasi, mamlaka, tabia na matendo ya viongozi mbalimbali yanavyoweza kujenga taswira ya uongozi wa kidini katika riwaya.

Osajie (2021) alichunguza majukumu ya viongozi wa dini katika jamii ya Nigeria. Walibainisha kuwa viongozi wa dini wana majukumu yanayozidi kuhubiri na kuongoza ibada, kwani wanatarajiwa pia kuwaelekeza waumini kuhusu masuala ya kisiasa na kijamii. Kwa mfano, alisisitiza umuhimu wa viongozi hao kuwa na uelewa wa mbinu na mivutano ya kisiasa ili waweze kuwaongoza waumini katika kufanya maamuzi ya uongozi. Pia alisisitiza kuwa viongozi wa dini wanapaswa kutambua na kuonya dhidi ya viongozi wenye mielekeo ya ugaidi, ubaguzi wa kidini, ukabila na upendeleo wa kijamii.

Ingawa Osajie hakujikita katika matini ya kifasihi, utafiti wao unaonyesha matarajio ya jamii kuhusu kiongozi wa dini kama mshauri na mwelekezi katika masuala yanayopita mipaka ya ibada. Mtazamo huu ni muhimu katika uchanganuzi wa kifasihi kwa sababu hutoa msingi wa kulinganisha wajibu unaotarajiwa wa kiongozi wa dini na matendo anayofanya ndani ya matini. Utafiti wao ulijikita katika majukumu ya viongozi wa dini katika kubadilisha jamii ya Nigeria,

wakati utafiti huu unachanganua namna majukumu na tabia hizo zinavyosawiriwa kisanaa katika *Paradiso*.

Nyandiri (2020) alichunguza nafasi ya dini katika kuhamasisha jamii na kutoa mafunzo kuhusu maadili. Katika mjadala wao kuhusu viongozi wa dini, walibaini kuwa baadhi yao wamekosa uaminifu na hali hiyo imechangia kuenea kwa ufisadi ndani ya taasisi za kidini. Fedha zilizokusudiwa kuwasaidia maskini, kwa mfano, zinaweza kutumiwa na watu walio katika nafasi za uongozi kwa manufaa yao wenyewe. Kwa mtazamo wake, uaminifu wa viongozi wa dini ungeweza kuiwezesha dini kutekeleza wajibu wake wa kuboresha maisha ya watu na kupunguza umaskini.

Utafiti huu unaonyesha mvutano kati ya uongozi wa kidini kama huduma na uongozi wa kidini kama nafasi ya kujinufaisha. Hata hivyo, Grégoire, Lachance na Taylor walijikita zaidi katika mchango wa viongozi wa dini katika kupambana na umaskini, wala hawakuchanganua ujenzi wa viongozi hao katika matini ya fasihi. Utafiti huu unatumia mtazamo wa kifasihi kuchunguza namna sifa na matendo ya viongozi wa dini yanavyoweza kuunda maana zinazokinzana ndani ya *Paradiso*.

Agboadanno na Dossouou (2018) walichunguza usawiri wa manabii wa uongo katika kazi ya Amma Darko. Walibaini kuwa viongozi hao hutumia mbinu mbalimbali kuwavuta watu katika ibada zao na hatimaye kuwatumia kama chanzo cha kujipatia utajiri. Miongoni mwa mbinu hizo ni kujitokeza wakati wa majanga, kutumia marejeleo ya Biblia na kudai uwezo wa kufanya miujiza. Kwa mtazamo wa watafiti hawa, matumizi hayo ya dini yanaonyesha jinsi viongozi wanaodai kuwa watumishi wa Mungu wanavyoweza kutumia mamlaka ya kidini kwa manufaa binafsi.

Utafiti wa Agboadanno na Dossouou ni muhimu zaidi kwa utafiti huu kwa sababu ulijikita katika kazi ya fasihi na ulionyesha namna mhusika kiongozi wa dini anavyoweza kusawiriwa kwa kinaya. Hata hivyo, ulijikita katika kazi ya Amma Darko na hasa katika manabii wa uongo, ilhali utafiti huu unachanganua viongozi wa dini katika riwaya ya Kiswahili *Paradiso*. Kwa hiyo, utafiti huu unaendeleza mjadala huo katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili na kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi.

Atieno (2019), katika tasnifu yake, alichunguza utambulisho wa jinsia katika riwaya *Maumbile si Huja* na *Paradiso*. Katika utafiti wake alibaini kuwa viongozi wa dini, ambao wanatarajiwa kuwa vielelezo vya maadili na kutoa mwelekeo kwa jamii, wanasawiriwa katika baadhi ya matukio kama wahusika wanaochangia kuzorota kwa maadili. Viongozi hao wanahusishwa na matendo kama usherati, ushirikina, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya. Aidha, baadhi yao wanahusishwa na msisitizo wa injili ya pesa, miujiza na utajiri badala ya malezi ya kiroho ya waumini.

Utafiti wa Atieno ni wa umuhimu wa moja kwa moja kwa utafiti huu kwa sababu, kama ilivyo katika utafiti huu, unahusisha *Paradiso* na unagusia namna viongozi wa dini wanavyosawiriwa. Hata hivyo, lengo kuu la Atieno lilikuwa utambulisho wa jinsia na aliongozwa na Nadharia ya Ufeministi. Utafiti huu unaweka usawiri wa viongozi wa dini kuwa mojawapo ya malengo yake mahsusi na unatumia Nadharia ya Udenguzi kuchunguza mikinzano na maana zinazojitokeza katika matini.

Big Mukolo (2020) anaonyesha uhusiano kati ya viongozi wa dini na watawala wenye mamlaka katika jamii. Kwa mujibu wa utafiti wake, manabii wa uongo au viongozi wa dini wanaotumikia maslahi binafsi wanaweza kushirikiana na watawala waovu ili kupata ulinzi na uhalali wa shughuli zao. Watawala nao hunufaika kwa kutumia viongozi hao kuwapofusha watu wasiweze kuhoji au kujitambua. Uhusiano huo hujengwa kupitia propaganda, miujiza ya uongo, ushirikina na mbinu nyingine zinazolenga kuwapumbaza na kuwatawala wanajamii.

Mjadala wa Big Mukolo unaonyesha kuwa usawiri wa kiongozi wa dini hauwezi kutenganishwa na mahusiano ya mamlaka katika jamii. Kiongozi anaweza kuonekana kama mwakilishi wa Mungu lakini wakati huohuo akawa sehemu ya mfumo unaowanyonya au kuwanyamazisha wanyonge. Hata hivyo, utafiti huo haukulenga moja kwa moja uchanganuzi wa *Paradiso* kama matini ya Kiswahili. Utafiti huu unatumia riwaya hiyo kuchanganua kwa kina namna uhusiano kati ya viongozi wa dini, waumini na mamlaka unavyojengwa na kujibomoa kimaana.

Nyandiri (2020) alichunguza changamoto zinazokabili uongozi wa makanisa nchini Kenya. Alibaini kuwa Wakenya wanawatarajia viongozi wa dini kutoa mwongozo wa kiroho na kijamii, lakini baadhi ya viongozi wamepoteza mwelekeo wa jukumu hilo. Migogoro ya uongozi, siasa ndani ya makanisa, rushwa, umaskini, kuibuka kwa madhehebu mengi na injili ya mafanikio vimetajwa kuwa miongoni mwa changamoto zinazoathiri uongozi wa dini. Kwa mujibu wa utafiti

huo, baadhi ya viongozi wamehusika katika siasa, migogoro na rushwa, hali inayohatarisha nafasi ya kanisa kama wakala wa mabadiliko na mtetezi wa wanyonge.

Nyandiri anaweka mjadala katika mazingira ya Kenya na hivyo kuongeza mtazamo wa ndani kuhusu matarajio na changamoto za viongozi wa dini. Hata hivyo, utafiti wake ni wa kijamii na hauchanganui namna viongozi hao wanavyosawiriwa katika kazi ya fasihi. Utafiti huu unatumia matokeo hayo kama msingi wa kutambua sifa ambazo jamii inatarajia kutoka kwa viongozi wa dini, kisha kuchanganua namna matarajio hayo yanavyothibitishwa au kupingwa katika *Paradiso*.

Osajie (2021) alichunguza viongozi wa dini kama mawakala wa amani na usalama kwa maendeleo endelevu nchini Nigeria. Alibainisha kuwa viongozi wa dini wana wajibu wa kukabiliana na maovu kama rushwa, ufisadi, upendeleo, ukandamizaji na mmomonyoko wa maadili. Kwa mtazamo wake, viongozi wa dini wanapaswa kusema ukweli bila woga au upendeleo, kukosoa viongozi wanaokiuka haki na sheria, na kuwa walinzi wa utu na maadili ya jamii. Pia alisisitiza kuwa mafundisho ya viongozi wa dini yanaweza kusaidia kurekebisha tabia za wananchi na kukuza uwajibikaji.

Utafiti wa Osajie unaonyesha upande mwingine wa usawiri wa viongozi wa dini, yaani kiongozi kama mlinzi wa maadili na mkosoaji wa maovu ya jamii. Mtazamo huu ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu unatoa msingi wa kulinganisha kiongozi anayetekeleza wajibu wake na kiongozi anayekiuka wajibu huo. Tofauti kubwa ni kwamba Osajie alichunguza jukumu la viongozi wa dini katika mazingira halisi ya Nigeria, wakati utafiti huu unachanganua ujenzi wa taswira hiyo katika matini ya *Paradiso*.

Zuhri na wenzake (2021) walichunguza nafasi ya viongozi wa dini katika uwezeshaji wa jamii. Walibaini kuwa viongozi hao wana nafasi katika masuala ya kidini, kijamii na kitaifa kwa kuwa wanaweza kuhamasisha, kutoa mwongozo na kuwahimiza wanajamii kushiriki katika shughuli za maendeleo. Viongozi wa dini pia walionekana kuwa na uwezo wa kuwasilisha sera kwa jamii na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika michakato ya maendeleo. Matokeo haya yanaonyesha taswira chanya ya kiongozi wa dini kama mshauri, mhamasishaji na kiungo kati ya jamii na taasisi nyingine.

Tofauti na tafiti zilizosisitiza uozo na matumizi mabaya ya mamlaka, Zuhri na wenzake wanaonyesha upande wa kiongozi wa dini anayetekeleza wajibu wake kwa jamii. Hata hivyo,

utafiti wao ulijikita katika uwezeshaji wa jamii na haukuwa uchanganuzi wa kifasihi. Utafiti huu unatumia mtazamo huo chanya kama sehemu ya kulinganisha na taswira nyingine za viongozi wa dini zinazojitokeza katika *Paradiso*.

Akong'o (2022) alichunguza tamaa na athari zake katika jamii kwa kuhakiki *Ua la Faraja* na *Paradiso*. Alibaini kuwa tamaa ya uongozi na mali ndani ya kanisa inaweza kuzalisha chuki, migogoro na ushindani miongoni mwa viongozi wa dini. Baadhi ya viongozi huoneana wivu kutokana na tamaa ya madaraka na kutaka kuhodhi waumini. Aidha, alionyesha kinaya ambapo taasisi ya dini inayotarajiwa kuleta amani na kusaidia kutatua matatizo ya ndoa inaweza kugeuka chanzo cha migogoro na kuvunjika kwa ndoa.

Utafiti wa Akong'o una umuhimu wa moja kwa moja kwa utafiti huu kwa sababu ulihusisha *Paradiso* na ulionyesha namna tamaa ya viongozi inavyoweza kubadili maana na nafasi ya taasisi ya dini. Hata hivyo, Akong'o alijikita katika tamaa kama suala kuu, wakati utafiti huu unachunguza kwa upana zaidi sifa, matendo, mamlaka na mahusiano ya viongozi wa dini katika kujenga taswira yao.

Njenga (2021) alichunguza uongozi katika fasihi ya kisasa kwa kurejelea *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso*. Alibaini kuwa baadhi ya viongozi wa dini katika riwaya hizo, badala ya kuwachunga waumini, wanawapotosha. Viongozi hao wanahusishwa na maisha ya ubadhirifu yanayotokana na rasilimali za wanyonge na msisitizo wa fedha badala ya imani. Pia, matendo yao yanaweza kuwafanya baadhi ya watu kuondoka au kukatishwa tamaa na taasisi ya dini.

Utafiti wa Njenga ni muhimu kwa sababu unahusisha moja kwa moja *Paradiso* na unaonyesha mabadiliko ya taswira ya kiongozi kutoka mlezi wa waumini hadi mhusika anayehusishwa na upotoshaji na ubadhirifu. Hata hivyo, Wanjiru alijikita katika suala pana la uongozi na aliongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya. Utafiti huu unatofautiana kwa kuweka mkazo mahsusi katika viongozi wa dini na kutumia Nadharia ya Udenguzi kuchanganua mikinzano inayojitokeza katika usawiri wao.

Muli (2024) alichunguza athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana kwa kulinganisha *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*. Utafiti wake ulibaini kuwa migogoro ya madhehebu, matumizi mabaya ya matoleo, umiliki wa maabadi kama mali za familia na matumizi ya nafasi za kidini kwa manufaa binafsi ni miongoni mwa mambo yanayowatamausha vijana. Pia alionyesha kuwa baadhi ya

viongozi wa dini huhusishwa na rushwa na matumizi ya madaraka kwa manufaa yao na ya familia zao. Viongozi hawa, ambao wanatarajiwa kuwa vielelezo vya maadili, wanaweza hivyo kusawiriwa kinyume na matarajio hayo.

Muli ana umuhimu wa pekee kwa utafiti huu kwa sababu alichanganua *Paradiso* na kugusia moja kwa moja tabia na matendo ya viongozi wa dini. Hata hivyo, mkazo wake ulikuwa katika udhanaishi wa kidini na athari zake kwa vijana, wakati utafiti huu unalenga kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini wenyewe. Kwa mtazamo wa Udenguzi, utafiti huu una nafasi ya kuchunguza zaidi mikinzano kati ya utambulisho wa viongozi kama watumishi wa dini na matendo yanayowasilishwa katika matini.

Muslim Councili of Elders (2024) ilijadili nafasi ya viongozi wa dini katika jamii ya kisasa na kubainisha kuwa viongozi hao wana ushawishi mkubwa katika mitazamo, tabia na maadili ya wanajamii. Walielezwa kama watetezi wa haki za kijamii, walinzi wa maadili na watetezi wa makundi yaliyo hatarini kama wanawake, watoto na maskini. Aidha, walionyeshwa kuwa na uwezo wa kushirikiana na taasisi za serikali na kutumia ushawishi wao kukabiliana na ubaguzi, ukosefu wa usawa, ghasia, ufisadi na rushwa.

Mtazamo wao unaendeleza upande chanya wa mjadala kuhusu viongozi wa dini kwa kuwa unasisitiza wajibu wao wa kijamii na kimaadili. Hata hivyo, kama tafiti nyingine za kijamii zilizopitiwa katika sehemu hii, haukulenga namna kiongozi wa dini anavyojengwa kama mhusika wa kifasihi. Kwa hiyo, utafiti huu unatumia matarajio hayo ya kijamii kama msingi wa kuchanganua namna matini ya *Paradiso* inavyoyathibitisha, kuyapindua au kuyakinza kupitia usawiri wa viongozi wake wa dini.

Kwa jumla, tafiti zilizopitiwa zinaonyesha kuwa viongozi wa dini wamesawiriwa au kujadiliwa katika mihimili miwili mikuu. Kwa upande mmoja, viongozi hawa wanaonekana kama walezi wa kiroho, walinzi wa maadili, wasuluhishi wa migogoro, watetezi wa haki na wawezeshaji wa jamii, kama inavyoonekana katika tafiti kama za Uttah na wenzake (2015), Osajie (2021) na Zuhri na wenzake (2021). Kwa upande mwingine, tafiti za Ng'etich (2011), Mosha (2013), Grégoire, Lachance na Taylor (2016) na Agboadanno na zinaonyesha taswira ya viongozi wanaohusishwa na dhuluma, unafiki, tamaa, matumizi mabaya ya mamlaka, ufisadi, ulaghai na upotoshaji wa waumini. Hivyo, mapitio yanaonyesha wazi kuwa usawiri wa kiongozi wa dini katika fasihi

unaweza kujengwa kwa mkinzano kati ya wajibu anaotarajiwa kuutekeleza na matendo anayotekeleza.

Pamoja na maendeleo hayo, kuna pengo linalojitokeza. Tafiti chache zimechanganua kwa kina jinsi matini ya riwaya inavyounda na kubomoa taswira ya kiongozi wa dini kupitia lugha, matendo, mahusiano, mamlaka na mikinzano ya ndani ya matini. Aidha, ingawa *Paradiso* tayari imefanyiwa tafiti na Ng'etich (2011), Atieno (2019), Akong'o (2022), Njenga (2021) na Muli (2024), tafiti hizo zimejikita katika masuala mahsusi kama dhuluma, jinsia, tamaa, uongozi na udhanaishi wa kidini. Bado kuna nafasi ya kuchanganua kwa mtazamo mahsusi wa Nadharia ya Udenguzi namna viongozi wa dini wanavyosawiriwa kwa maana zinazokinzana na zinazoibua taswira ambazo hazibaki thabiti ndani ya *Paradiso*. Pengo hili ndilo linalolengwa na utafiti huu.

2.2.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii

Katika utafiti huu, maadili ya jamii yanaeleweka kama kanuni, misingi na mienendo inayotumika kuongoza mahusiano na tabia za wanajamii. Dini ni mojawapo ya taasisi zinazohusishwa na ujenzi na uendelezaji wa maadili kwa kuwa mafundisho ya kidini huweka misingi kuhusu mema na mabaya, wajibu wa mtu kwa wengine, uadilifu, huruma na uwajibikaji. Hata hivyo, katika fasihi dini haisawiriwi kwa namna moja tu. Waandishi wanaweza kuonyesha namna dini inavyosaidia kuimarisha maadili, lakini pia wanaweza kuonyesha hali ambapo taasisi au wahusika wa kidini wanapotenda kinyume na misingi wanayoihubiri, jambo linaloweza kusababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kwa msingi huo, mapitio haya yanazingatia tafiti zinazoonyesha uhusiano kati ya dini, mienendo ya wahusika na mabadiliko ya kimaadili katika jamii.

Mungah (1999) alichunguza masuala ya kidini na kifalsafa katika kazi za fasihi za Kiswahili, akibainisha namna imani na mitazamo ya kidini inavyohusiana na maisha ya binadamu. Utafiti wake unaonyesha kuwa dini inaweza kuwa chanzo cha mwongozo wa kimaisha na namna ya kuelewa matukio yanayowakabili wanajamii. Mtazamo huu ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu unaonyesha upande chanya wa dini katika kuunda mitazamo na mienendo ya jamii. Hata hivyo, utafiti huo haukutilia mkazo wa kutosha namna matendo ya taasisi za kidini yanavyoweza kuzalisha au kuathiri mienendo inayopingana na misingi ya maadili. Utafiti huu unapanua mjadala huo kwa kuchunguza namna taswira ya dini katika *Paradiso* inavyojengwa na wakati huohuo kuvurugwa kupitia matendo na kauli za wahusika.

Magare (2002) alijadili masuala ya kidini katika fasihi ya Kiswahili na kuonyesha nafasi ya imani katika maisha ya wahusika. Utafiti wake unaashiria kuwa dini huathiri namna wahusika wanavyotafsiri maisha, mateso na wajibu wao katika jamii. Ingawa utafiti huo unatoa msingi wa kuelewa nafasi ya dini katika maisha ya kijamii, haukuangazia kwa kina athari za mgongano kati ya mafundisho ya dini na vitendo vya wafuasi wake katika ujenzi wa maadili. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu unachunguza namna mgongano huo unavyojitokeza katika *Paradiso* na namna unavyoweza kusababisha maana ya dini kutokuwa thabiti.

Browning na Cooper (2004) walijadili masuala ya imani na uzoefu wa binadamu katika fasihi, wakionyesha namna wahusika wanavyokabiliana na changamoto za maisha huku wakihusisha uzoefu wao na imani. Mtazamo huu unaonyesha kuwa dini inaweza kuwa nyenzo ya kumsaidia mwanadamu kupata mwelekeo wa kimaadili wakati wa kukabili matatizo. Hata hivyo, utafiti huo haukuchanganua kwa kina hali ambapo dini yenyewe inaweza kuhusishwa na migogoro ya kimaadili katika jamii. Kwa hiyo, utafiti huu unaongeza mwelekeo mwingine kwa kuchunguza si tu nafasi ya dini katika kuwapa wahusika mwongozo, bali pia namna inavyoweza kuhusishwa na vitendo vinavyopingana na maadili yanayodaiwa kuwakilishwa nayo.

Mose (2005) alichunguza masuala ya kidini na kifalsafa katika fasihi, akionyesha namna wahusika wanavyopitia migogoro inayohusisha imani, maisha na hali zao za kijamii. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa masuala ya imani yanaweza kuwa sehemu muhimu ya migogoro inayowakabili wanadamu. Ingawa utafiti huu unasaidia kuelewa uhusiano kati ya dini na maisha ya kijamii, haukuweka mkazo mahsusi kwenye athari za dini katika maadili ya jamii. Utafiti wa sasa unatofautiana kwa kuifanya athari hiyo kuwa sehemu mahsusi ya uchanganuzi, huku ukichunguza pia mikinzano inayojitokeza kati ya misingi ya kidini na matendo ya wahusika.

Mbatiah (2001) alijadili namna fasihi inavyowasilisha masuala ya kijamii na kiimani yanayowakabili wanadamu. Utafiti wake unaonyesha kuwa fasihi inaweza kutumika kufichua migogoro inayotokana na tofauti kati ya matarajio ya jamii na hali halisi ya maisha. Mwelekeo huu ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa *Paradiso* pia inawasilisha hali ambamo matarajio ya jamii kuhusu dini yanakabiliwa na matendo yanayopingana nayo. Hata hivyo, utafiti wa Mbatiah haukulenga moja kwa moja kuchanganua namna dini inavyoathiri maadili ya jamii kwa mtazamo wa Udenguzi. Utafiti huu unaziba pengo hilo kwa kuangalia namna maana ya dini na maadili inavyoundwa na kuvunjwa ndani ya matini.

Ogutu (2013) alichunguza masuala ya kijamii na kiitikadi katika fasihi ya Kiswahili na kubainisha namna kazi za fasihi zinavyowasilisha migongano inayotokea katika jamii. Utafiti wake una umuhimu katika kuelewa kwamba fasihi haiakisi tu maadili yaliyopo bali pia huhoji misingi inayoyaunda. Hata hivyo, utafiti huo haukuweka dini kama kipengele kikuu cha kuchunguza athari zake katika maadili ya jamii. Kwa upande wake, utafiti huu unalenga kubainisha namna dini inavyohusishwa na mabadiliko ya kitabia na kimaadili katika *Paradiso,* na namna mikinzano hiyo inavyofichua maana zinazopingana ndani ya matini.

Matundura (2019) alichunguza masuala yanayohusu maisha na mitazamo ya jamii katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wake unaonyesha namna matini za kifasihi zinavyoweza kuibua changamoto zinazowakabili wanajamii na kuhoji misingi ya mienendo yao. Ingawa mtazamo huo una uhusiano na utafiti huu katika suala la kuchunguza changamoto za kimaadili, haukuweka mkazo mahsusi kwenye athari ya dini katika maadili ya jamii. Kwa hiyo, utafiti huu unatofautiana kwa kuunganisha vipengele viwili, yaani dini na maadili, na kuvichanganua kwa kutumia misingi ya Udenguzi.

Chimerah (2021) alijadili masuala ya kijamii na kiimani katika fasihi ya Kiswahili, akionyesha namna imani inavyohusiana na maisha na mienendo ya wahusika. Utafiti huo una umuhimu kwa kuonyesha kuwa masuala ya dini yanaweza kutumiwa na mwandishi kufichua hali mbalimbali za jamii. Hata hivyo, haukuweka mkazo wa kutosha kwenye swali la iwapo dini huimarisha au hudhoofisha maadili ya jamii kupitia matendo ya wahusika na taasisi zinazoiwakilisha. Utafiti huu unalenga kuchunguza suala hilo kwa kina katika *Paradiso* kwa kuangalia mikinzano kati ya mafundisho ya dini, matarajio ya jamii na matendo yanayowasilishwa katika riwaya.

Kwa jumla, tafiti zilizopitiwa zinaonyesha kuwa dini ni kipengele muhimu katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu inahusishwa na imani, mwenendo, migogoro ya kijamii na namna wahusika wanavyotafsiri maisha. Hata hivyo, sehemu kubwa ya tafiti hizi imejikita katika masuala mapana ya dini, imani, falsafa, mateso na migogoro ya kijamii, badala ya kuchanganua moja kwa moja athari za dini katika maadili ya jamii. Aidha, tafiti hizo hazijaweka mkazo wa kutosha katika kuchunguza namna dini inavyoweza kuwasilishwa kwa maana mbili zinazokinzana, yaani kama chanzo cha maadili na wakati huohuo kama chanzo cha vitendo vinavyoyadhoofisha. Hapa ndipo utafiti huu unapojiweka kwa kuchanganua *Paradiso* kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi ili

kubainisha namna maana ya dini na athari zake katika maadili inavyojengwa, kupingwa na kujibomoa ndani ya matini.

2.3 Msingi wa Nadharia

Sehemu hii inajadili nadharia inayotumika kuongoza utafiti huu. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Udenguzi, ambayo inafaa katika kuchanganua namna maana hujengwa, hutofautiana na wakati mwingine kujibomoa ndani ya matini ya kifasihi. Nadharia hii inatoa msingi wa kuchunguza mikinzano, utata na maana zinazoweza kujitokeza katika usawiri wa dini, viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii katika riwaya teule. Udenguzi hauishii katika kubainisha maana iliyo wazi ya matini, bali huchunguza pia mikinzano iliyomo ndani yake na namna vipengele mbalimbali vya matini vinavyoweza kuathiri au kubadili maana hiyo. Katika utafiti huu, nadharia hiyo inatumika kwa kuzingatia mihimili iliyoteuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Kama inavyoelezwa katika maandiko yaliyotangulia, Udenguzi hulenga kufichua mikinzano na maana zilizofichika katika matini badala ya kuichukulia kazi ya fasihi kuwa na maana moja isiyobadilika.

2.3.1 Nadharia ya Udenguzi

Nadharia ya Udenguzi ni mkabala wa kifalsafa na kiuhakiki unaosisitiza uchunguzi wa kina wa matini ili kubainisha mikinzano na kuyumbayumba kwa maana. Mkabala huu unapingana na mtazamo unaodhani kuwa matini ina maana moja ya mwisho inayoweza kufikiwa kwa urahisi. Badala yake, Udenguzi huchunguza namna lugha inavyounda maana na jinsi maana hiyo inaweza kubadilika kutokana na uhusiano wa ishara, kauli na dhana zinazotumiwa katika matini. Kwa mtazamo huu, matini inaweza kutoa maana zaidi ya moja, hata pale ambapo inaonekana kuwa mwandishi ametoa msimamo mmoja ulio wazi. Katika fasihi, hivyo, mhakiki huzingatia si tu kile kinachosemwa na matini, bali pia mikinzano, mapengo na mambo ambayo matini yenyewe huyafichua bila kukusudia.

Nadharia hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu suala la dini katika *Paradiso* linaweza kuwasilishwa kupitia mitazamo inayokinzana. Dini inaweza kuonekana kama chanzo cha mwongozo wa kimaadili, lakini matendo ya baadhi ya wahusika wanaoiwakilisha yanaweza kuibua picha tofauti. Vivyo hivyo, viongozi wa dini wanaweza kutarajiwa kuwa vielelezo vya maadili, lakini matendo yao katika matini yanaweza kuibua maswali kuhusu uadilifu wao. Kwa

hiyo, Udenguzi unamwezesha mtafiti kutosheka na maana ya juu juu ya dini, bali kuchunguza namna matini inavyojenga na kuvuruga maana hiyo kupitia mikinzano yake ya ndani.

Kwa mujibu wa Derrida (1967), Udenguzi ni hatua tokezi ya Ubadamuundo, ambapo Derrida alihoji dhana ya *logocentrism* katika falsafa ya Ulaya. Mtazamo huu unahusisha uchunguzi wa imani kwamba kuna chanzo au msingi mkuu unaoweza kutoa maana ya mwisho. Mulokozi anaonyesha pia kuwa Derrida alitilia shaka kuwepo kwa uhusiano wa kidaraja kati ya usemaji na uandishi, akisisitiza kuwa kila mmoja unaweza kuwa na muktadha na uwezo wake wa kuwasilisha maana.

Kwa upande mwingine, Miller (1967) anaeleza kuwa Udenguzi si tendo la kuivunja kazi ya fasihi vipandevipande kutoka nje, bali ni mchakato wa kubainisha namna matini yenyewe inavyojivunja kutokana na mikinzano iliyomo ndani yake. Hivyo, udenguzi si uharibifu wa matini bali ni uchunguzi unaofichua namna matini inavyojenga maana na wakati huohuo kutoa dalili zinazoweza kuipinga maana hiyo. Mtazamo huu una umuhimu katika utafiti huu kwa sababu unamwezesha mtafiti kuchunguza iwapo taswira ya dini inayojengwa katika *Paradiso* inaendelea kuwa thabiti au inajenga mikinzano inayoweza kuibadilisha.

Aidha, Udenguzi unapinga mgawanyiko mkali wa hali mbili zinazowekwa kama zinazopingana, kama vile mwili/roho, uzuri/ubaya na juu/chini. Badala yake, nadharia huonyesha kuwa pande hizo zinaweza kutegemeana na kuchangiana katika ujenzi wa maana. Katika matini ya kifasihi, kwa hiyo, kinachoonekana kuwa kizuri kinaweza kuwa na kipengele cha ubaya, na kinachoonekana kuwa cha kweli kinaweza kubeba dalili zinazokifanya kitiliwe shaka. Mtazamo huu ni muhimu katika *Paradiso* kwa kuwa unaruhusu kuchunguza kwa kina mikinzano kati ya mafundisho ya dini na matendo ya wanaodai kuyafuata.

Kwa jumla, Nadharia ya Udenguzi inampa utafiti huu msingi wa kuchunguza *Paradiso* kama matini yenye maana zinazoweza kujengwa na kuvurugwa kwa wakati mmoja. Hata hivyo, utafiti huu hautumii kila dhana inayohusishwa na Udenguzi. Badala yake, unateua mihimili inayohusiana moja kwa moja na malengo yake matatu. Kabla ya kueleza mihimili hiyo, ni muhimu kufafanua uhasisi na uendelezaji wa Nadharia ya Udenguzi, ili kuweka msingi wa kihistoria na kifalsafa wa nadharia inayotumika katika utafiti huu.

2.3.1.1 Uhasisi na Uendelezaji wa Nadharia ya Udenguzi

Nadharia ya Udenguzi iliasisiwa na mwanafalsafa Mfaransa Jacques Derrida katika miaka ya 1960. Msingi wa fikra za Udenguzi uliibuka katika mazingira ya mijadala ya kifalsafa na kiulimi iliyokuwa ikihoji mitazamo iliyodhani kuwa lugha ina mfumo thabiti unaoweza kutoa maana isiyobadilika. Derrida aliendeleza mjadala huu kwa kuhoji dhana kwamba kuna msingi mmoja wa mwisho unaoweza kuthibitisha maana ya matini. Kwa mtazamo wake, maana huendelea kuzalishwa kupitia uhusiano wa ishara na ishara nyingine, hivyo haiwezi kufungwa katika tafsiri moja ya mwisho. Maelezo haya yanaendana na mtazamo kwamba Udenguzi unachunguza namna lugha na maana zinavyoingiliana na jinsi matini inavyoweza kubeba maana zinazokinzana.

Uhasisi wa Udenguzi ulihusishwa kwa kiasi kikubwa na kazi za Derrida za mwishoni mwa miaka ya 1960, hususan *Of Grammatology*, *Writing and Difference* na *Speech and Phenomena*. Kupitia maandiko hayo, Derrida alihoji baadhi ya misingi iliyokuwa imejengwa na falsafa ya Kimagharibi kuhusu lugha, uwepo, ukweli na maana. Alielekeza mjadala kwenye kile alichokiita *logocentrism*, yaani mwelekeo wa kutafuta msingi mkuu au chanzo cha mwisho cha maana. Kwa mujibu wa Mulokozi (2002), Derrida aliijenga hoja yake kwa kuonyesha kuwa usemaji na uandishi haviwezi kuwekwa katika uhusiano wa kidaraja ambapo kimoja kinachukuliwa kuwa bora au chenye mamlaka zaidi kuliko kingine.

Ingawa Derrida ndiye anayehusishwa moja kwa moja na uhasisi wa Udenguzi, fikra zake hazikuibuka katika ombwe la kifalsafa. Zilijengwa pia kutokana na mijadala ya wanafalsafa waliomtangulia, wakiwamo Hegel, Nietzsche, Freud, Heidegger na Husserl. Wanafalsafa hawa walitoa mijadala mbalimbali kuhusu lugha, maarifa, uwepo, fahamu na namna binadamu anavyoufikia ukweli. Derrida alichukua baadhi ya maswali haya na kuyasoma upya kwa kuyaweka katika mtazamo unaosisitiza tofauti, ukinzani na kutokuwepo kwa msingi wa mwisho wa maana. Kwa hiyo, Udenguzi unaweza kueleweka kama sehemu ya mwendelezo wa mjadala mpana wa kifalsafa kuhusu uwezekano wa kupata maana au ukweli ulio thabiti.

Katika maendeleo yake, Udenguzi ulihusishwa pia na Umuundo, ingawa ulijitokeza kama mkabala wa kuhoji baadhi ya misingi ya Umuundo. Umuundo uliweka mkazo katika mifumo ya lugha na mahusiano ya vipengele vinavyounda mfumo huo. Udenguzi, kwa upande wake, ulihoji uwezekano wa mfumo huo kutoa maana iliyofungwa na thabiti. Kwa mujibu wa Njogu na

Chimerah, Udenguzi unapinga mitazamo inayochukulia lugha na fasihi kuwa miundo inayojitawala yenyewe. Aidha, tofauti na mtazamo wa Saussure uliosisitiza zaidi usinkronia, Udenguzi unaweza kuhusisha usinkronia na udiakronia katika kuchunguza mabadiliko na mahusiano yanayozalisha maana.

Dhana muhimu iliyojengeka katika maendeleo ya Udenguzi ni kwamba maana haifungwi katika ishara moja. Ishara hupata maana kutokana na uhusiano wake na ishara nyingine, na uhusiano huo unaweza kuendelea bila kufikia kituo cha mwisho cha maana. Kwa sababu hiyo, Udenguzi huzingatia hali ya *tofauti* na *uahirishaji wa maana*. Miller (1967) anaeleza kwamba udenguzi hauishii katika kubomoa matini, bali huonyesha namna matini yenyewe inavyojenga na kujivunja kutokana na mikinzano yake ya ndani. Hivyo, udenguzi ni mchakato wa kujenga upya uelewa wa matini baada ya kubainisha mikinzano iliyofichika ndani yake.

Kadiri ulivyoendelea kutumika, Udenguzi ulipanuka kutoka mijadala ya kifalsafa na kuwa mkabala muhimu katika uhakiki wa fasihi. Wahakiki walianza kuutumia kuchunguza jinsi matini zinavyounda maana, jinsi zinavyoweka dhana katika jozi zinazopingana na jinsi matini hizo zinavyoweza kutoa dalili zinazopinga madai yao wenyewe. Katika usomaji wa kiudenguzi, kwa hiyo, mhakiki haishii katika kutafuta ujumbe mkuu wa mwandishi, bali huchunguza pia kile ambacho matini inakifanya kuwa tata, kinachopingana na kinachobaki bila kutatuliwa. Mtazamo huu unafanya Udenguzi kuwa muhimu katika utafiti wa masuala yenye utata kama dini, kwa kuwa unaruhusu kuchunguza kwa pamoja maana zinazokinzana zinazojengwa ndani ya matini.

Katika fasihi ya Kiswahili, Udenguzi umeendelea kutumiwa katika kuchanganua matini na vipengele mbalimbali vya lugha na fasihi. Hivyo, maendeleo ya nadharia hii hayakuishia katika mazingira yake ya awali ya kifalsafa, bali yaliingia katika taaluma ya fasihi kama mkabala wa kusoma upya matini na kubainisha mikinzano yake. Utafiti huu unaendeleza mkondo huo kwa kuitumia Nadharia ya Udenguzi kuchanganua taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii katika *Paradiso*. Hata hivyo, kwa kuwa utafiti huu hauwezi kutumia kila dhana ya Udenguzi kwa wakati mmoja, sehemu inayofuata inafafanua mihimili ya nadharia hii na kuonyesha misingi inayoweza kutumika katika uchanganuzi wa matini.

2.3.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Udenguzi

Nadharia ya Udenguzi ina dhana na misingi mbalimbali inayomwezesha mhakiki kuchunguza namna maana inavyojengwa na kuvurugwa katika matini. Mihimili hiyo haipaswi kuchukuliwa kama orodha iliyofungwa ya kanuni za nadharia hii, kwa kuwa Udenguzi unahusisha dhana mbalimbali kama vile kutokuwa thabiti kwa maana, mikinzano ya ndani ya matini, tofauti na uahirishaji wa maana, pamoja na kuhoji misingi inayodaiwa kuwa na mamlaka ya mwisho katika ufasiri. Kwa mujibu wa mtazamo wa Udenguzi, matini inaweza kuwa na maana zaidi ya moja na maana hizo zinaweza hata kukinzana.

Katika utafiti huu, mihimili mitatu imeteuliwa kutokana na uhusiano wake wa moja kwa moja na malengo ya utafiti. Mhimili wa kwanza unahusu kutokuwepo kwa toleo la mwisho la kazi ya fasihi; wa pili unahusu kuwepo kwa maana mbalimbali zinazokinzana katika matini; na wa tatu unahusu kutopatikana kwa maana katika ishara moja pekee bali kuwepo kwa hali ya kuwepo na kutokuwepo. Mihimili hii ndiyo itakayowezesha utafiti kuchanganua taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

Mhimili wa kwanza: Hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Mhimili huu unasisitiza kuwa kazi ya fasihi haiwezi kufungwa katika fasiri moja ya mwisho. Matini inaweza kusomwa kwa mitazamo mbalimbali na kila usomaji unaweza kufichua maana ambayo haikujitokeza katika usomaji mwingine. Kwa mtazamo huu, mhakiki anapaswa kuwa tayari kuchunguza matini kwa kina badala ya kudhani kwamba maana iliyo wazi ndiyo maana pekee inayowezekana. Miller (1967) anaeleza kuwa Udenguzi hufichua namna kazi ya fasihi inavyojivunja yenyewe kutokana na mikinzano iliyomo ndani yake. Katika utafiti huu, mhimili huu utaongoza **lengo la kwanza**, ambalo ni kuchanganua taswira ya dini katika riwaya teule. Utasaidia kuchunguza taswira mbalimbali za dini zinazojengwa katika *Paradiso* na kubainisha iwapo taswira hiyo inaweza kueleweka kwa maana moja tu au kama matini inaruhusu fasiri zinazotofautiana.

Mhimili wa pili: Matini ya fasihi huwa na maana mbalimbali zinazokinzana. Mhimili huu unatokana na dhana kwamba matini inaweza kujenga maana mbili au zaidi ambazo hazikubaliani kikamilifu. Udenguzi hauchukulii ukinzani huo kama dosari ya matini, bali huufanya kuwa sehemu muhimu ya uchanganuzi. Hivyo, mhakiki huchunguza namna matini inavyowasilisha upande mmoja kuwa wenye mamlaka na wakati huohuo kutoa dalili zinazoweza kuupinga.

Udenguzi pia hupinga mgawanyiko mkali wa jozi kinzani kwa kuonyesha kuwa pande hizo zinaweza kutegemeana katika ujenzi wa maana. Katika utafiti huu, mhimili huu utaongoza lengo la pili, ambalo ni kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini. Utatumika kubainisha mikinzano kati ya nafasi inayotarajiwa ya viongozi wa dini kama waelekezi wa maadili na namna wanavyosawiriwa kupitia kauli, matendo na mahusiano yao katika *Paradiso*.

Mhimili wa tatu: Maana haipatikani katika ishara moja pekee, bali huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo. Mhimili huu unatokana na wazo kwamba maana ya ishara haijitoshelezi yenyewe, bali hujitokeza kupitia uhusiano wake na ishara nyingine. Kwa hiyo, kile kinachoonekana kuwepo katika matini kinaweza pia kubeba dalili za kutokuwepo kwake au kuhojiwa kwake. Maana huendelea kusogezwa na kubadilika badala ya kufikia kituo kimoja cha mwisho. Mtazamo huu unaendana na maelezo kwamba Udenguzi hutofautisha na kuahirisha maana ya viashiria na kwamba kila usomaji unaweza kuzalisha uelewa mpya wa matini. Katika utafiti huu, mhimili huu utaongoza lengo la tatu, ambalo ni kubainisha athari za dini katika maadili ya jamii. Utasaidia kuchunguza namna dini inavyohusishwa na ujenzi wa maadili, lakini pia namna matendo na matukio katika *Paradiso* yanavyoweza kuonyesha kudhoofika, kupingana au kutokuwepo kwa maadili yanayodaiwa kuhusishwa na dini.

Kwa hiyo, mihimili hii mitatu inahusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Mhimili wa kwanza unalenga utofauti wa taswira ya dini, wa pili unalenga mikinzano katika usawiri wa viongozi wa dini, na wa tatu unalenga mabadiliko na mikinzano ya maana inayohusisha dini na maadili ya jamii. Mgawanyo huu unaiwezesha nadharia kutumika kama chombo cha uchanganuzi badala ya kuwa maelezo ya kinadharia pekee. Hata hivyo, kabla ya kuonyesha kwa undani jinsi mihimili hii itakavyotumika katika utafiti, ni muhimu kupitia tafiti za kifasihi zilizowahi kutumia Nadharia ya Udenguzi.

2.3.1.3 Tafiti za Kifasihi Zilizotumia Nadharia ya Udenguzi

Nadharia ya Udenguzi imekuwa ikitumika katika uhakiki wa fasihi kuchunguza namna matini zinavyojenga maana na wakati huohuo kutoa dalili zinazoweza kupinga maana hiyo. Katika maendeleo ya uhakiki wa kifasihi, nadharia hii ilihusishwa na wahakiki wa Shule ya Yale, wakiwamo Hartman, de Man, Miller na Bloom, ambao waliitumia katika uchanganuzi wa matini za kifasihi. Baadaye, mkabala huu ulipanuka na kutumika katika tafiti za fasihi ya Kiafrika na

Kiswahili kuchunguza masuala kama mamlaka, utambulisho, jinsia na mahusiano ya kijamii. Njogu na Chimerah (1999), kwa mfano, wanaonyesha umuhimu wa Udenguzi katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili, hususan katika kuchunguza namna lugha inavyoweza kuzalisha maana zinazotofautiana.

Murithi (2015) alitumia mtazamo wa kiudenguzi katika kuchanganua methali za Kiswahili. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu ulihamisha Udenguzi kutoka katika mjadala wa kifalsafa na kuutumia katika kuchunguza kipengele mahususi cha lugha ya Kiswahili. Kwa mtazamo huu, methali hazichukuliwi kuwa na maana moja iliyofungwa, bali huchunguzwa kwa kuzingatia mahusiano na mikinzano inayoweza kujitokeza katika maana zake. Utafiti huo una umuhimu kwa utafiti huu kwa kuwa unaonyesha uwezekano wa kutumia Udenguzi katika mazingira ya Kiswahili na kuchunguza maana zinazojengwa kupitia lugha. Hata hivyo, tofauti na Murithi aliyejikita katika methali, utafiti huu unachanganua matini ya kinathari, yaani riwaya, kwa kuzingatia taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

Aidha, tafiti zilizotumia Udenguzi katika fasihi zimeonyesha kuwa nadharia hii inaweza kutumika kufichua maana zinazokinzana ndani ya matini. Katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili, mtazamo huu ni muhimu kwa sababu matini inaweza kuonekana kutoa msimamo mmoja, lakini uchunguzi wa ndani ukaonyesha dalili zinazoukinza msimamo huo. Kwa mfano, matini inaweza kumwasilisha mhusika kama mwadilifu kupitia kauli zake, lakini matendo yake yakafichua kinyume cha sifa hiyo. Hali hii ndiyo msingi wa usomaji wa kiudenguzi unaolenga kubainisha namna matini inavyojenga na kujibomoa yenyewe.

Katika eneo la dini, Ng'etich (2011) alichunguza dini kama chombo cha kuwadhulumu waumini katika *Paradiso, Nguvu ya Sala, Nitaolewa Nikipenda* na *Masaibu ya Ndugu Jero*. Utafiti huo ulibaini aina mbalimbali za dhuluma zinazohusishwa na dini, zikiwamo za kisaikolojia, kiuchumi, kifamilia, kimwili na kiakili. Muhimu zaidi, utafiti huo ulionyesha kinaya kwamba dini, ambayo inatarajiwa kuwa kimbilio la waumini na chombo cha kukuza maadili na umoja wa kijamii, inaweza pia kutumiwa kuwadhulumu. Mtazamo huu una uhusiano mkubwa na utafiti huu kwa sababu unadhihirisha kuwepo kwa mgongano kati ya matarajio yanayohusishwa na dini na matendo yanayofanywa kwa jina la dini. Hata hivyo, Ng'etich alilenga zaidi dhuluma za kidini, ilhali utafiti huu unachanganua kwa upana zaidi taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii, kwa kutumia mihimili mahususi ya Udenguzi.

Utafiti wa Karanja (2005) nao una umuhimu katika muktadha huu kwa kuwa ulichunguza nafasi ya dini katika jamii ya kisasa kama ilivyosawiriwa katika riwaya kadhaa za Kiswahili. Karanja alibaini kuwa dini imepoteza baadhi ya nafasi yake ya awali katika jamii na kwamba baadhi ya watu wameifikisha katika hali ya kupoteza uaminifu wake kutokana na kushindwa kutoa suluhisho kwa matatizo ya maisha. Matokeo hayo yanaonyesha kuwepo kwa mvutano kati ya dhima inayotarajiwa ya dini na namna inavyoonekana katika maisha ya jamii. Ingawa utafiti wa Karanja haukulenga *Paradiso* pekee wala haukujikita katika malengo matatu ya utafiti huu, unaweka msingi muhimu wa kuisoma dini kama dhana yenye maana zinazoweza kubadilika na kukinzana.

Utafiti unaohusisha moja kwa moja dini, *Paradiso* na Udenguzi ni wa Ng'etich, ambao unaonyesha namna dini inavyoweza kudenguliwa kama chombo cha kuwadhulumu waumini. Utafiti huo ulibaini kwamba dini inayotarajiwa kuwa nyenzo ya kukuza maadili na umoja inaweza pia kutumiwa na baadhi ya viongozi na waumini kuwadhulumu wenzao. Hata hivyo, kuwepo kwa utafiti huo hakumaanishi kwamba suala la dini katika *Paradiso* limehitimishwa. Badala yake, unaonyesha uwezekano wa kuendelea kulichunguza kwa mtazamo mpana zaidi wa kiudenguzi. Utafiti huu unatofautiana kwa kuchanganua kwa pamoja vipengele vitatu vinavyohusiana, yaani taswira ya dini, viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

Kwa ujumla, tafiti zilizotumia Nadharia ya Udenguzi zinaonyesha kuwa mkabala huu unafaa katika kuchanganua matini ambazo zina mikinzano ya ndani na maana zisizoweza kufungwa katika fasiri moja. Tafiti za Kiswahili pia zimethibitisha kuwa Udenguzi unaweza kutumika katika kuchanganua lugha na matini za kifasihi, huku utafiti wa Ng'etich ukionyesha umuhimu wake katika kuchunguza dini kama eneo lenye mgongano kati ya matarajio na uhalisia. Hata hivyo, tafiti zilizopitiwa hazijaunganisha kwa kina taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii katika uchanganuzi mmoja wa riwaya ya *Paradiso*. Hivyo, utafiti huu unaendeleza matumizi ya Udenguzi kwa kuuchagua na kuhusisha mihimili mitatu mahsusi na malengo yake matatu. Hii ndiyo itakayofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

2.3.1.4 Mihimili ya Udenguzi Iliyotumika katika Utafiti Huu

Ingawa Nadharia ya Udenguzi ina dhana na mikabala mbalimbali, utafiti huu umechagua mihimili mitatu inayohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Uchaguzi huu unalenga kuhakikisha kuwa nadharia haitumiki kwa ujumla bila kuhusishwa na maswali mahsusi ya utafiti. Mihimili

hiyo inatumika kuchanganua namna matini ya *Paradiso* inavyojenga, kupinga na kubadilisha maana kuhusu dini, viongozi wa dini na maadili ya jamii. Uteuzi wa mihimili hiyo unatokana na msingi kwamba Udenguzi huzingatia maana zinazotofautiana, mikinzano ya ndani ya matini na kutokuwepo kwa maana ya mwisho.

Mhimili wa kwanza: Hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Mhimili huu ulitumika katika kutekeleza lengo la kwanza, ambalo ni kuchanganua taswira ya dini katika riwaya teule. Katika uchanganuzi, mtafiti hakuchukulia kwamba *Paradiso* inatoa taswira moja ya dini inayoweza kufungwa katika maana moja. Badala yake, mtafiti alitafuta namna taswira hiyo inavyojengwa kupitia kauli, matendo, wahusika na matukio mbalimbali, kisha akachunguza iwapo vipengele hivyo vinaunga mkono au vinakinzana na taswira inayojengwa. Kwa mtazamo huu, dini inaweza kusawiriwa kama chanzo cha imani, mwongozo na maadili, lakini matini inaweza wakati huohuo kutoa dalili zinazoifanya taswira hiyo itiliwe shaka. Mhimili huu, kwa hiyo, unamwezesha mtafiti kutoa fasiri inayotokana na ushahidi wa matini bila kudai kuwa hiyo ndiyo fasiri pekee inayowezekana. Udenguzi unasisitiza kwamba kazi ya fasihi inaweza kufasiriwa kwa zaidi ya njia moja na kwamba matini inaweza kujenga maana zinazokinzana.

Mhimili wa pili: Matini ya fasihi huwa na maana mbalimbali zinazokinzana. Mhimili huu ulitumika katika kutekeleza lengo la pili, ambalo ni kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini katika riwaya teule. Mtafiti alichunguza mgongano kati ya nafasi inayotarajiwa ya kiongozi wa dini na namna kiongozi huyo anavyosawiriwa katika matini. Kwa mfano, kiongozi wa dini anaweza kutarajiwa kuwa mwadilifu, mwaminifu na mlezi wa maadili, lakini matendo yake yakadhihirisha tamaa, ubinafsi, unafiki au matumizi mabaya ya mamlaka. Badala ya kuchagua upande mmoja kuwa ndio maana pekee, mhimili huu unaruhusu kuchanganua pande zote mbili na kubainisha namna zinavyotegemeana katika ujenzi wa maana. Hivyo, usawiri wa kiongozi wa dini unaweza kueleweka kama eneo ambalo matini inajenga maana na wakati huohuo inaiweka katika hali ya mashaka. Mtazamo huu unaendana na msingi wa Udenguzi kwamba matini inaweza kuwa na maana mbalimbali zinazokinzana.

Mhimili wa tatu: Maana haipatikani katika ishara moja pekee, bali huwa katika hali ya kuwepo na kutokuwepo. Mhimili huu ulitumika katika kutekeleza lengo la tatu, ambalo ni kubainisha athari za dini katika maadili ya jamii. Mtafiti alichunguza namna dhana ya maadili inavyowasilishwa kupitia dini na namna matendo ya wahusika yanavyoweza kuunga mkono au kupinga maadili

hayo. Kwa mfano, dini inaweza kuhusishwa na uadilifu, upendo, mshikamano na kuwajibika kwa jamii, lakini matendo yanayofanywa kwa kisingizio cha dini yanaweza kuonyesha ubaguzi, unyonyaji, udanganyifu au ukosefu wa haki. Kwa hiyo, maana ya dini kama chanzo cha maadili haiwezi kutenganishwa na dalili zinazoonyesha kudhoofika kwa maadili hayo. Mhimili huu humwezesha mtafiti kuchunguza si kile kinachoonekana kuwepo katika matini pekee, bali pia kile ambacho matini inakifanya kuwa hakipo, kinachokosekana au kinachopingwa. Hii inaendana na dhana ya Udenguzi kwamba maana huendelea kutofautishwa na kuahirishwa badala ya kufikia kituo cha mwisho.

Kwa msingi huo, matumizi ya mihimili hii katika utafiti yanafuata mnyororo wa kimantiki unaounganisha nadharia, lengo na uchanganuzi wa matini. Mhimili wa kwanza unasaidia kufungua uwezekano wa fasiri mbalimbali za taswira ya dini; mhimili wa pili unafichua mikinzano inayojitokeza katika usawiri wa viongozi wa dini; na mhimili wa tatu unasaidia kuchunguza uhusiano unaobadilika kati ya dini na maadili ya jamii. Kwa namna hii, Nadharia ya Udenguzi haitumiki kama maelezo ya jumla katika sura ya pili pekee, bali inakuwa chombo cha uchanganuzi kitakachorejelewa katika Sura ya Nne wakati wa kuhusisha ushahidi wa *Paradiso* na malengo ya utafiti. Hili ni muhimu kwa sababu watahini walisisitiza kwamba mihimili iliyotajwa katika Sura ya Pili lazima ionekane ikifanya kazi katika uchanganuzi wa data, si kubaki katika maelezo ya kinadharia pekee.

2.4 Hitimisho

Sura hii imejadili maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti pamoja na msingi wa kinadharia unaoongoza utafiti huu. Mapitio ya maandishi yamepangwa kwa kuzingatia malengo matatu ya utafiti. Kwanza, maandishi kuhusu taswira ya dini katika fasihi yameonyesha kuwa dini inaweza kuwasilishwa kama mfumo wa kiimani na kimaadili, lakini pia kama taasisi ya kijamii inayohusishwa na masuala ya mamlaka, utajiri na maslahi binafsi. Pili, tafiti kuhusu usawiri wa viongozi wa dini zimeonyesha mvutano kati ya matarajio ya jamii kwa viongozi hao na matendo yao, ambapo wanaweza kuwasilishwa kama walezi wa kiroho na waadilifu, lakini pia kama wahusika wenye unafiki, tamaa, matumizi mabaya ya mamlaka na maslahi binafsi. Tatu, maandishi kuhusu athari za dini katika maadili ya jamii yameonyesha uhusiano kati ya dini, maisha ya jamii, mitazamo ya watu na mwenendo wa kimaadili. Pamoja na mchango wa tafiti hizo, imebainika kuwa bado kuna pengo katika kuchanganua kwa pamoja taswira ya dini, usawiri wa

viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii katika riwaya *Paradiso* kwa mtazamo wa Nadharia ya Udenguzi.

Kwa upande wa kinadharia, sura hii imejadili uhasisi na uendelezaji wa Nadharia ya Udenguzi, misingi yake pamoja na matumizi yake katika uhakiki wa kifasihi. Nadharia hii inatoa mtazamo unaowezesha kuchunguza namna maana zinavyojengwa, zinavyokinzana na wakati mwingine kujibomoa ndani ya matini, badala ya kudhani kuwa matini ina maana moja ya mwisho na isiyobadilika. Katika utafiti huu, mihimili mitatu imechaguliwa kwa kuzingatia uhusiano wake wa moja kwa moja na malengo ya utafiti. Mhimili wa kutokuwepo kwa toleo la mwisho la kazi ya fasihi utaongoza uchanganuzi wa taswira ya dini; mhimili wa kuwepo kwa maana mbalimbali zinazokinzana katika matini utaongoza uchanganuzi wa usawiri wa viongozi wa dini; na mhimili wa kutopatikana kwa maana katika ishara moja pekee, bali katika hali ya kuwepo na kutokuwepo, utaongoza uchanganuzi wa athari za dini katika maadili ya jamii. Kwa msingi huo, Udenguzi utatumika kama mkabala wa kuchunguza mikinzano, tofauti na kutokuwa thabiti kwa maana zinazojitokeza kupitia lugha, wahusika, matendo na mahusiano katika *Paradiso*.

Kwa jumla, mapitio ya maandishi na mjadala wa kinadharia umebainisha kuwa ingawa tafiti zilizopo zimejadili dini, viongozi wa dini na maadili katika miktadha mbalimbali ya kifasihi na kijamii, bado kuna haja ya kuchunguza namna masuala hayo yanavyohusiana na kujenga maana zinazokinzana ndani ya matini moja kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi. Utafiti huu unakusudia kuziba pengo hilo kwa kuchanganua taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii katika *Paradiso*. Msingi wa kinadharia uliowekwa katika sura hii utaendelea kutumika katika Sura ya Nne wakati wa kuchanganua data, ambapo kila mhimili utarejelewa kwa kuhusishwa na lengo lake husika. Hivyo, utafiti utaweza kubainisha namna *Paradiso* inavyojenga, kupinga na wakati mwingine kujibomoa yenyewe katika uwasilishaji wa dini na nafasi yake katika maisha na maadili ya jamii.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza mbinu na taratibu zilizotumika katika kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data ya utafiti. Kwa kuwa utafiti huu ni wa kifasihi na umejikita katika uchanganuzi wa matini ya riwaya ya *Paradiso* (Habwe, 2005), ulitumia mkabala wa kithamano pamoja na muundo wa kimaelezo. Sura hii inawasilisha muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, uthabiti na kuaminika kwa data, maadili ya utafiti na hitimisho la sura.

3.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpango na mkakati unaoongoza namna utafiti unavyotekelezwa ili kufikia malengo yaliyowekwa (Kumar, 2011). Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ndani ya mkabala wa kithamano. Muundo wa kimaelezo humwezesha mtafiti kueleza na kufasiri sifa, matukio na maana zinazojitokeza katika data bila kutegemea vipimo vya kitakwimu. Kwa upande mwingine, mkabala wa kithamano hujikita katika data za maneno na maana zinazojitokeza kutokana na muktadha wa jambo linalochunguzwa.

Katika utafiti huu, mkabala wa kithamano ulifaa kwa sababu data kuu zilitokana na matini ya kifasihi, yaani riwaya ya *Paradiso*. Data hizo zilihusisha dondoo, kauli, matendo ya wahusika na matukio yanayohusiana na taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii. Data hizo hazikuhitaji kupimwa kwa kutumia takwimu bali zilihitaji kusomwa, kutafsiriwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia muktadha wa matini.

Muundo wa kimaelezo uliteuliwa kwa sababu ulimwezesha mtafiti kueleza kwa kina namna vipengele vya dini vinavyojitokeza katika riwaya na namna maana zake zinavyojengwa, kukinzana na kuvurugwa ndani ya matini. Hivyo, muundo wa utafiti ulikuwa wa kimaelezo, mkabala wa utafiti ulikuwa wa kithamano, uchanganuzi wa data ulifanywa kwa njia ya kimaelezo kwa kuongozwa na mihimili teule ya Nadharia ya Udenguzi, na uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya kimaelezo kwa kutumia dondoo kutoka katika riwaya kama ushahidi.

Muundo huu uliwezesha utafiti kufikia malengo yake kwa kutoa nafasi ya kuchunguza maana mbalimbali za dini ndani ya matini na kubainisha mikinzano inayojitokeza katika ujenzi wa taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti linaweza kurejelea mazingira ya kitaaluma ambamo utafiti unafanywa. Kwa utafiti huu, eneo la kitaaluma ni Fasihi ya Kiswahili, hususan utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Eneo hili liliteuliwa kwa sababu utafiti unahusu uchanganuzi wa taswira ya dini katika matini ya kifasihi, ambapo masuala ya dini, viongozi wa dini na maadili ya jamii yanajengwa kupitia matumizi ya lugha, wahusika, matukio na mbinu mbalimbali za kifasihi.

Kimazingira, utafiti ulifanywa maktabani. Mtafiti alitumia maktaba kupata na kusoma riwaya teule pamoja na vitabu, tasnifu, makala za majarida na maandiko mengine ya kitaaluma yaliyohusiana na mada ya utafiti. Hata hivyo, chanzo kikuu cha data ya utafiti kilikuwa riwaya ya *Paradiso* (Habwe, 2005), huku machapisho mengine yakitumika zaidi kama vyanzo vya upili katika kujenga msingi wa kitaaluma na kinadharia wa utafiti.

3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa ni jumla ya vitu au matini zenye sifa zinazohusiana na jambo linalochunguzwa na ambazo mtafiti anakusudia kuzihusisha na utafiti wake (Best na Kahn, 2009). Kwa kuwa utafiti huu ni wa kifasihi, kundi lengwa halihusishi watu bali linahusisha riwaya za Kiswahili zinazoshughulikia masuala ya dini, maadili ya jamii na uongozi wa kidini.

Kundi hili lilichaguliwa kwa kuzingatia uhusiano wake na mada ya utafiti. Riwaya zinazoshughulikia dini zinaweza kujenga taswira mbalimbali za dini, kuwasawiri viongozi wa dini kwa namna tofauti na kuonyesha athari za taasisi na imani za kidini katika maisha na maadili ya jamii. Kwa hiyo, kundi lengwa lilitoa msingi mpana ambao kutoka kwake matini iliyofaa kwa madhumuni ya utafiti ingeweza kuteuliwa.

Katika utafiti huu, riwaya ya *Paradiso* si kundi lengwa bali ni sampuli ya matini iliyoteuliwa kutoka katika kundi hilo.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ni sehemu ya kundi lengwa inayoteuliwa kwa ajili ya kuchunguzwa kwa kina (Kumar, 2011). Usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa kwa kuzingatia vigezo vinavyohusiana na madhumuni ya utafiti (Kombo na Tromp, 2006).

Utafiti huu ulitumia usampulishaji dhaminifu katika kuteua riwaya ya *Paradiso* (Habwe, 2005). Riwaya hii iliteuliwa kwa sababu inaangazia masuala ya dini kwa namna inayohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Matini hiyo ina nafasi ya kuchunguza taswira mbalimbali za dini, usawiri wa viongozi wa dini na uhusiano kati ya dini na maadili ya jamii.

Uteuzi wa riwaya moja uliruhusu mtafiti kufanya usomaji wa kina wa matini badala ya kufanya uchanganuzi wa juu juu wa matini nyingi. Kwa kuwa madhumuni ya utafiti yalilenga uchanganuzi wa kifasihi wa *Paradiso*, mtafiti alijikita katika matini hiyo moja ili kuchunguza kwa kina vipengele vilivyolengwa na utafiti.

Kwa hiyo, kundi lengwa lilikuwa riwaya za Kiswahili zinazoshughulikia dini, maadili na uongozi wa kidini, ilhali sampuli ilikuwa riwaya ya *Paradiso* (Habwe, 2005), iliyoteuliwa kimakusudi kwa kutumia usampulishaji dhaminifu.

3.5 Ukusanyaji Data

Ukusanyaji wa data ni mchakato wa kupata taarifa zinazohitajika ili kutimiza malengo ya utafiti (Kothari, 2004). Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa kutumia usomaji makini wa matini, huku riwaya ya *Paradiso* ikiwa chanzo kikuu cha data.

Ukusanyaji wa data ulifanyika kwa hatua kadhaa. Kwanza, mtafiti aliisoma riwaya ya *Paradiso* kwa makini zaidi ya mara moja ili kuifahamu kwa kina na kubaini maeneo yaliyohusiana na mada ya utafiti. Pili, wakati wa usomaji, mtafiti alitambua dondoo, kauli, matendo ya wahusika na matukio yaliyohusiana na malengo matatu ya utafiti. Tatu, data zilizobainishwa zilinakiliwa katika daftari la kunukuu data na kupangwa katika makundi kulingana na lengo husika. Nne, dondoo hizo zilihifadhiwa na kupangwa kwa ajili ya hatua ya uchanganuzi.

Data ziliainishwa katika makundi matatu makuu yanayolingana na malengo ya utafiti. Kundi la kwanza lilihusisha dondoo zinazohusu taswira ya dini. Kundi la pili lilihusisha dondoo zinazohusu usawiri wa viongozi wa dini. Kundi la tatu lilihusisha dondoo zinazohusu athari za dini katika maadili ya jamii.

Mtafiti pia alirejelea vitabu, tasnifu, makala za majarida na maandiko mengine ya kitaaluma yaliyohusiana na mada. Vyanzo hivi vilitumika kama data za upili katika kuimarisha uelewa wa mada na kusaidia katika mjadala wa matokeo.

3.6 Uchanganuzi wa data

Vifaa vya utafiti ni nyenzo zinazomwezesha mtafiti kukusanya, kuhifadhi na kupanga data kwa utaratibu unaofaa. Katika utafiti huu, vifaa vilivyotumika vilikuwa riwaya ya *Paradiso*, daftari la kunukuu data, kalamu na jedwali la uchanganuzi wa data.

Riwaya ya *Paradiso* ilikuwa chanzo kikuu cha data. Daftari la kunukuu data lilitumika kurekodi dondoo na taarifa muhimu zilizobainishwa wakati wa usomaji. Kalamu ilitumika katika kurekodi na kupanga data wakati wa mchakato wa usomaji. Jedwali la uchanganuzi lilitumika kupanga dondoo kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi iliyoteuliwa.

Jedwali la uchanganuzi lilijumuisha, miongoni mwa vipengele vingine, dondoo kutoka katika matini, ukurasa wa dondoo, lengo husika, kipengele kinachochanganuliwa, mhimili wa Udenguzi unaohusika na tafsiri ya mtafiti. Mpangilio huu ulimwezesha mtafiti kufuatilia chanzo cha kila data na kuhakikisha kuwa dondoo zilizokusanywa zinahusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti.

Vifaa hivi vilisaidia kuweka data katika mfumo unaoweza kufuatiliwa kutoka katika matini asilia hadi katika uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo.

3.7 Uthabiti wa data

Uchanganuzi wa data ni mchakato wa kuzipanga, kuzitafsiri na kuzihusisha data na maswali au malengo ya utafiti. Katika utafiti huu, data zilichanganuliwa kwa mkabala wa kimaelezo kwa kuongozwa na mihimili mitatu teule ya Nadharia ya Udenguzi.

Uchanganuzi ulifuata hatua kadhaa. Kwanza, dondoo zilizokusanywa wakati wa usomaji zilisomwa tena kwa kina ili kuhakikisha kuwa zilihusiana na malengo ya utafiti. Pili, dondoo ziliainishwa kulingana na malengo matatu ya utafiti. Tatu, kila dondoo lilihusishwa na mhimili wa Nadharia ya Udenguzi uliofaa kulifasiri. Nne, mtafiti alichanganua maana zilizojengwa katika dondoo, mikinzano iliyojitokeza na namna matini ilivyoweza kujenga na wakati huohuo kuvuruga maana fulani. Tano, uchanganuzi ulihusishwa na tafiti na mawazo ya wataalamu yaliyopitiwa katika Sura ya Pili ili kuonyesha ulinganifu, tofauti au mchango wa matokeo ya utafiti.

Katika kuchanganua data, mtafiti hakujikita katika kusimulia matukio ya riwaya pekee. Badala yake, alizingatia namna matini inavyojenga maana, inavyowasilisha mikinzano na namna maana hizo zinavyoweza kubadilika au kuvurugwa. Hivyo, dondoo kutoka katika riwaya zilitumika kama ushahidi wa hoja za uchanganuzi.

Matokeo ya uchanganuzi yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo katika Sura ya Nne. Uwasilishaji huo ulipangwa kulingana na malengo ya utafiti na uliambatanishwa na dondoo kutoka katika *Paradiso* kama ushahidi wa hoja zilizochanganuliwa.

3.7.1 Usahihi wa data

Uthabiti wa data katika utafiti wa kithamano unahusisha kuhakikisha kuwa mchakato wa ukusanyaji, upangaji na uchanganuzi wa data unafanyika kwa utaratibu unaoweza kufuatiliwa na kutoa matokeo yanayoendana na data asilia. Katika utafiti huu, uthabiti wa data uliimarishwa kwa kutumia matini asilia ya *Paradiso* kama chanzo kikuu, kusoma matini hiyo kwa makini zaidi ya mara moja na kurekodi dondoo kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

Aidha, dondoo zilizokusanywa zilihakikiwa dhidi ya matini asilia ili kuhakikisha kuwa zilinukuliwa kwa usahihi na kwamba maana yake haikubadilishwa. Data ziliwekwa katika makundi kulingana na malengo ya utafiti na kila dondoo lilipewa rejeleo la ukurasa wa matini ili kurahisisha uthibitishaji wake.

Uthabiti uliimarishwa pia kwa kuhakikisha kuwa hatua za uchanganuzi zilifuata utaratibu uleule katika malengo yote matatu. Data ziliainishwa, zikahusishwa na mhimili unaofaa wa Udenguzi, zikatafsiriwa na kisha kuhusishwa na lengo husika. Aidha, uchanganuzi wa data ulijadiliwa na msimamizi wa utafiti ili kupata maoni ya kitaaluma kuhusu uhusiano kati ya data, malengo na nadharia.

3.7.2 Kuaminika kwa data za utafiti

Kuaminika kwa data katika utafiti wa kithamano kunahusu kiwango ambacho matokeo ya utafiti yanaweza kutegemewa kutokana na namna data zilivyokusanywa, kuthibitishwa na kuchanganuliwa (Golafshani, 2003). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutegemea matini asilia ya *Paradiso* na kwa kufanya usomaji wa kina wa riwaya hiyo mara kadhaa.

Mtafiti alihakikisha kuwa dondoo zilizotumika katika uchanganuzi zilitokana moja kwa moja na matini teule na kwamba hazikubadilishwa ili kuendana na mawazo ya mtafiti. Kila dondoo liliangaliwa katika muktadha wake ndani ya riwaya kabla ya kutumiwa katika uchanganuzi. Aidha, data ziliainishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuhusishwa na mihimili mahususi ya Nadharia ya Udenguzi.

Kuaminika kwa uchanganuzi kuliongezwa kwa kulinganisha tafsiri ya data na maudhui ya matini pamoja na mjadala wa kitaaluma katika Sura ya Pili. Pale ambapo kulikuwa na uwezekano wa tafsiri zaidi ya moja, mtafiti alizingatia muktadha wa matini na ushahidi wa ndani wa riwaya badala ya kulazimisha maana moja. Hatua hizi zilisaidia kuhakikisha kuwa matokeo yaliyojitokeza yalitokana na ushahidi wa matini na si mawazo ya mtafiti pekee.

3.8 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti yanahusu kanuni zinazomwongoza mtafiti katika kuhakikisha kuwa mchakato wa utafiti unafanywa kwa uaminifu, uwajibikaji na kwa kuzingatia taratibu za kitaaluma. Kwa kuwa utafiti huu ni wa kithamano na unahusu uchanganuzi wa matini, maadili yake yalijikita zaidi katika uaminifu wa kitaaluma, matumizi sahihi ya vyanzo, kunukuu kwa usahihi, kutopotosha maana ya matini na kuheshimu haki za mwandishi.

Mtafiti alitumia riwaya ya *Paradiso* kama chanzo kikuu cha data na alihakikisha kuwa dondoo zilizotumiwa katika uchanganuzi zilitolewa kwa usahihi kutoka katika matini. Hakubadilisha wala kupotosha kauli za mwandishi ili kuendana na hoja zake. Vyanzo vya kitaaluma vilivyotumiwa katika utafiti vilirejelewa kwa kufuata utaratibu wa kitaaluma wa utoaji wa marejeleo.

Aidha, mtafiti alizingatia kaida na taratibu za kitaaluma zilizowekwa na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki (CUEA) katika utekelezaji wa utafiti. Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa matini na haukuhusisha wahojiwa au ukusanyaji wa taarifa binafsi kutoka kwa watu, mtafiti alizingatia hasa uadilifu wa kitaaluma, uaminifu katika kunukuu matini na matumizi sahihi ya vyanzo.

Mtafiti pia alihakikisha kuwa kazi za watafiti wengine hazikunakiliwa bila kutambuliwa. Mawazo, hoja na matokeo yaliyochukuliwa kutoka kwa wataalamu wengine yalirejelewa ipasavyo. Hatua hizi zililenga kudumisha uadilifu wa kitaaluma na kuhakikisha kuwa uchanganuzi wa *Paradiso* unawasilishwa kwa uaminifu bila kupotosha matini au vyanzo vilivyotumika.

3.9 Hitimisho la Sura ya Tatu

Sura hii imeeleza mbinu na taratibu zilizotumika katika kutekeleza utafiti. Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo ndani ya mkabala wa kithamano, huku eneo la utafiti likiwa Fasihi ya Kiswahili, hususan riwaya ya Kiswahili. Kundi lengwa lilihusisha riwaya za Kiswahili zinazoshughulikia masuala ya dini, maadili na uongozi wa kidini, ambapo *Paradiso* iliteuliwa kama sampuli kwa kutumia usampulishaji dhaminifu. Sura pia imeeleza hatua za ukusanyaji na uchanganuzi wa data, vifaa vilivyotumika, namna uthabiti na kuaminika kwa data kulivyohakikishwa pamoja na maadili yaliyofuatwa. Mbinu hizi ziliuwezesha utafiti kukusanya na kuchanganua data kutoka katika *Paradiso* kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili teule ya Nadharia ya Udenguzi.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha data ya uchanganuzi wa riwaya *Paradiso* ya John Habwe kwa kuzingatia malengo matatu ya utafiti. Lengo la kwanza ni kuchanganua taswira ya dini, la pili ni kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini, na la tatu ni kubainisha athari za dini katika maadili ya jamii. Uwasilishaji wa matokeo umefuata mpangilio wa malengo hayo ili kuweka uhusiano wa moja kwa moja kati ya malengo ya utafiti, ushahidi wa matini na mjadala wa matokeo.

Uchanganuzi umejikita katika dondoo kutoka *Paradiso*, ambazo zimechanganuliwa kwa kuzingatia muktadha, wahusika, lugha na mahusiano yanayojitokeza katika matini. Dondoo hizo zimehusishwa na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi pamoja na tafiti zilizopitiwa katika Sura ya Pili. Kwa msingi huo, mjadala unalenga kubainisha maana, mikinzano na mitazamo mbalimbali inayojitokeza katika usawiri wa dini, viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Udenguzi, uchanganuzi unatilia mkazo namna matini inavyojenga na wakati huohuo kuyumbisha maana kuhusu dini. Hivyo, dini inaweza kuwasilishwa kwa maana zinazokinzana, kama chanzo cha matumaini, wokovu na mshikamano kwa upande mmoja, na kama inayohusishwa na migogoro, unyonyaji au mmomonyoko wa maadili kwa upande mwingine. Mikinzano hiyo ndiyo msingi wa kuchanganua namna maana kuhusu dini zinavyojengwa na kujibomoa ndani ya *Paradiso*.

4.1 Taswira ya Dini katika Riwaya ya *Paradiso*

Taswira ya dini katika sehemu hii inachanganuliwa kwa kuzingatia namna matini inavyolijenga wazo la dini kupitia matukio, wahusika, mazungumzo na mazingira ya kidini. Mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Udenguzi, unaosisitiza kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi, unafaa hapa kwa sababu taswira ya dini katika *Paradiso* haijengwi kwa maana moja. Matini inatoa taswira zinazotofautiana na wakati mwingine zinazopingana. Kwa hiyo, badala ya kutafuta hukumu moja kuhusu dini, uchanganuzi unaangalia namna taswira hizo zinavyojengwa na jinsi moja inavyoweza kuisumbua au kuipinga nyingine.

Matokeo yanaonyesha taswira kuu zifuatazo: dini kama chanzo cha tumaini; njia ya wokovu; chanzo cha miujiza na uponyaji; wito wa mtu; chanzo cha migogoro na utengano; mfumo wenye kanuni kali; chombo cha unyanyasaji na unyonyaji; na kichocheo cha maendeleo ya jamii. Mchanganyiko huu ndio unaoifanya taswira ya dini katika riwaya isiwe ya upande mmoja.

4.1.1 Dini kama Chanzo cha Tumaini

Habwe analijenga dini kama chanzo cha tumaini kupitia safari ya Michael ya kutafuta suluhisho la ugonjwa ambao haukuweza kutatuliwa kwa njia za kawaida. Mwanzoni, hospitali inashindwa kumpa Mango jibu la kuridhisha kuhusu hali ya mwanawe. Michael anahamisha tegemeo lake kutoka katika matibabu ya kawaida kwenda katika imani na maombi. Hivyo, tumaini linajengwa ndani ya matini kupitia mabadiliko ya mtazamo wa mhusika kuhusu uwezekano wa kupona.

Tukio hili linaonyesha kwamba dini inapata maana yake kutokana na uhusiano wake na hali ya kukata tamaa. Bila ugonjwa na kushindwa kwa mbinu nyingine, nafasi ya imani isingeonekana kwa nguvu hiyo. Kwa mtazamo wa Udenguzi, maana ya dini kama tumaini kwa hiyo inajengwa pamoja na kile kinachoonekana kuwa kinyume chake, yaani kutokuwa na uhakika na kushindwa kwa tiba za kawaida.

> *“Alining’iniza moyo wake kwenye maneno ya Yesu ambayo yalijaa tumaini. Alifahamu baba yake hakuwa mwumini. Baba yake alikuwa mithili ya kinyonga. Hana msimamo katika masuala ya itikadi kama haya. Michael alimheshimu lakini akaona yeye ataishi maisha tofauti Maulana akimpa uwezo wa kuishi…” (uk. 6).*

Hapa maneno “tumaini” na “ataishi” yanaonyesha kuwa imani ya Michael haijengwi kama maarifa yaliyokamilika, bali kama tegemeo linalompa uwezekano wa kutazama hali yake kwa namna tofauti. Aidha, kutajwa kwa baba yake kama mtu asiye na msimamo kunajenga upinzani kati ya imani ya mtoto na mtazamo wa baba. Upinzani huo unafanya maana ya dini kama tumaini ijitokeze kwa nguvu, lakini wakati huohuo unafichua kuwa tumaini linategemea mtazamo wa mhusika na mazingira yake.

Kwa hivyo, matini inajenga dini kama nafasi ya matumaini bila kuifunga katika tafsiri moja ya mwisho. Tumaini linakuwa na maana kwa sababu linasimama dhidi ya hali ya kutokuwa na uhakika inayomkabili Michael.

4.1.2 Dini kama Njia ya Wokovu

Taswira ya dini kama njia ya wokovu inajitokeza katika mabadiliko ya Mango baada ya kuona nafuu ya Michael. Mango anaunganisha tukio la uponyaji na imani ya Kikristo na hatimaye anakuwa muumini. Hapa dini inawasilishwa kama njia inayomwelekeza mhusika kutoka katika hali ya kutafuta msaada wa aina mbalimbali kwenda katika imani.

Hata hivyo, matini haijengi uongofu kama jambo lisilo na mvutano. Mango anapojaribu kumshawishi Zuhra ajiunge naye, Zuhra anakataa na kusisitiza kuwa uongofu ni uamuzi wa mtu. Mazungumzo haya yanazalisha maana mbili zinazokinzana: upande mmoja wokovu unaonekana kuwa wa lazima kwa mwamini, na upande mwingine hiari ya mtu inasisitizwa. Kwa mtazamo wa Udenguzi, maana ya "wokovu" kwa hiyo inatetereka kati ya wito wa kuamini na uhuru wa kukataa.

> *"Kwa sababu mume wako yuko kule na kuonyesha umoja wa nyumba na mwili inabidi kuabudu mahali pamoja." "Uongofu mume wangu ni uamuzi wa mtu." Zuhra alisema huku kidari kimejaa upepo wa hasira." (uk. 22).*

Jibu la Zuhra linadhoofisha dhana kwamba umoja wa familia lazima utolewe katika umoja wa kidini. Kwa hiyo, matini inajenga wazo la wokovu na wakati huo huo inafichua mipaka ya wazo hilo linapowekwa juu ya uhuru wa mtu mwingine. Huu ni mfano wa maana inayojijenga na kujivunja ndani ya mazungumzo hayo hayo.

Kwa jumla, wokovu katika *Paradiso* unaonekana kama uwezekano wa mabadiliko ya mtu, lakini matini inaacha wazi mvutano kati ya imani ya mtu na uhuru wa mwingine.

4.1.3 Dini kama Chanzo cha Miujiza na Uponyaji

Tukio la Michael kupona baada ya kuombewa ni mojawapo ya matukio yanayojenga dini kama chanzo cha miujiza. Ugonjwa wake unashindwa kutatuliwa na hospitali, kisha maombi yanahusishwa na nafuu yake. Tukio hilo linampa Michael mwelekeo mpya wa maisha na baadaye anaitikia wito wa huduma.

Taswira hii inaendelezwa pia kupitia Salome, ambaye baada ya kukaa muda mrefu bila kupata mtoto hatimaye anapata mtoto. Katika matukio yote mawili, muujiza unaunganishwa na mabadiliko makubwa katika maisha ya wahusika. Hata hivyo, Udenguzi unatuelekeza kutazama namna maana ya muujiza inavyotegemea mvutano kati ya kile kinachoonekana kuwa hakiwezekani na kile kinachotokea ndani ya matini.

“Mimi baba nimepata njozi ya ajabu. Hadi leo yapata mwezi mmoja Malaika wa Bwana amenitokea akaniambia napaswa kuiacha kazi ili nimtumikie kama muinjilisti.” (uk. 25).

Muujiza hapa hauishii katika kupona kwa mwili. Unazalisha mabadiliko ya utambulisho wa Michael. Hivyo, matini inaunganisha uponyaji na wito. Kwa upande mwingine, maana ya muujiza haiwezi kutenganishwa na imani ya wahusika wanaoutafsiri kama tendo la Mungu. Hivyo, matini inaruhusu usomaji unaoona tukio kama muujiza wa kidini na usomaji unaoliona kama tukio linalopata maana kupitia imani ya wahusika.

Kwa hiyo, taswira ya dini kama chanzo cha miujiza inajengwa kupitia matukio yanayobadilisha maisha ya wahusika, huku maana ya muujiza ikibaki wazi kwa tafsiri zaidi ya moja.

4.1.4 Dini kama Wito wa Mtu

Dini katika *Paradiso* pia inajengwa kama wito unaoweza kubadilisha mwelekeo wa maisha ya mtu. Musa anaacha ualimu na kuingia katika huduma, huku Michael akiacha kazi yake na kujiunga na huduma ya uinjilisti. Amuko naye anahusishwa na wito baada ya kupata msaada wa kiroho.

Matukio haya yanaonyesha kuwa wito unajengwa kama nguvu inayomfanya mhusika kubadili kazi, mahusiano na matarajio ya maisha. Hata hivyo, matini pia inaonyesha kuwa wito huo hauondoi udhaifu wa kibinadamu. Baadhi ya wahusika wanaoitikia wito baadaye wanahusishwa na migogoro na makosa. Kwa hiyo, dhana ya wito inajengwa na wakati huo huo inatetereka inapokutana na matendo ya wahusika.

“Musa kwa upande wake, aliacha kazi yake ya ualimu. Alikuwa Mwalimu Shule ya Machakos. Aliacha na kuingia katika huduma. Alikuwa amefundisha kwa miaka kumi.” (uk. 31).

Kauli hii inajenga uamuzi wa Musa kama tendo la kujitoa. Lakini kwa mtazamo wa Udenguzi, maana ya wito haiwezi kutengwa na matokeo ya baadaye ya maisha ya Musa. Mhusika huyu baadaye anahusishwa na matukio yanayopingana na taswira ya mtumishi mkamilifu. Hivyo, matini yenyewe inasumbua maana ya wito kama dhamana ya moja kwa moja ya uadilifu.

Kwa hivyo, wito katika riwaya unaonekana kuwa mwanzo wa safari ya kidini, lakini si dhamana ya tabia njema ya mhusika.

4.1.5 Dini kama Chanzo cha Migogoro na Utengano

Kinyume na taswira ya dini kama chombo cha kuunganisha watu, *Paradiso* inaonyesha dini ikiweza kuwa chanzo cha migogoro na utengano. Mgogoro wa uongozi katika New Jerusalem unasababisha mgawanyiko wa kanisa na waumini. Tofauti kati ya viongozi inahamishwa kutoka kiwango cha mawazo hadi kwenye mapambano ya wazi.

Tukio hili ni muhimu kwa Udenguzi kwa sababu linavuruga upinzani wa kawaida kati ya dini na migogoro. Dini ambayo inatarajiwa kuleta umoja inakuwa mazingira ya kuibuka kwa mgawanyiko. Kwa hiyo, maana ya umoja haionekani nje ya maana ya utengano, bali zote mbili zinajengwa ndani ya matini.

> *"Nyinyi mnaabudu Mungu gani? Sasa mnapigania nini? Polisi mmoja alimwuliza mama mmoja aliyekuwa amevunjwa mkono..." (uk. 77).*

Swali la polisi linafichua mkanganyiko wa msingi: watu wanaohusishwa na ibada wanajikuta wakipigana. Hapa matini inajiuliza kuhusu uhusiano kati ya kile kinachodaiwa na kile kinachofanyika. Dini kama chanzo cha amani inasukumwa pembeni na dini kama mazingira ya ushindani. Hivyo, taswira yake haikai katika upande mmoja.

Matini kwa hiyo inajenga dini kama taasisi yenye uwezo wa kuunganisha na pia kugawanya, jambo linalodhihirisha kutotulia kwa maana yake ndani ya riwaya.

4.1.6 Dini kama Mfumo Wenye Kanuni Kali

Dini pia inasawiriwa kama mfumo unaoweka kanuni kuhusu ndoa, ulevi, mahusiano na namna ya kuishi. Mango anakabiliwa na matarajio ya kanisa kuhusu wake wengi, ulevi na kimada. Vilevile, Michael anakabiliwa na ushauri wa kuoa licha ya kutaka kujitolea katika huduma bila ndoa.

Katika sehemu hii, mtafiti haishii kueleza kanuni hizo. Kinachochanganuliwa ni mkinzano unaojengwa kati ya kanuni rasmi na hali halisi ya wahusika. Mango tayari ana wake kadhaa kabla ya kuingia katika mfumo huo wa kidini. Hivyo, matini inakabiliwa na swali la iwapo maana ya ndoa inapaswa kufafanuliwa na kanuni ya taasisi au na hali halisi ya mahusiano ya kijamii.

> *"Kuna baadhi ya waumini walioona kuwa hastahili kuwa kiongozi akiwa na wake watano... Licha ya manung'uniko haya, Mango alishika hatamu hizi za uongozi..." (uk. 22).*

Ingawa waumini ndio msingi wa kanisa, sauti zao zinajitokeza kama manung'uniko yasiyo na nguvu, huku Mango akiendelea kuendesha ibada. Hapa kuna upinzani kati ya mamlaka ya kanuni na mamlaka inayotokana na utekelezaji wa madaraka. Matini inajenga matarajio ya kwamba kanuni ziwe na nguvu, lakini tukio lenyewe linaonyesha kuwa mamlaka ya vitendo inaweza kuzidi sauti ya kanuni. Aidha, dhana ya ndoa inakuwa na maana mbili: kanuni inajaribu kuweka mpaka wa ndoa halali, lakini matini wakati huo huo inakiri uwepo wa wake wa Mango. Hivyo, dhana hiyo haina maana moja thabiti ndani ya tukio.

Kwa hiyo, dini kama mfumo wa kanuni kali inajengwa na matini, lakini utekelezaji wake unafichua mipasuko na mikinzano inayofanya maana ya kanuni hizo isiwe ya mwisho.

4.1.7 Dini kama Chombo cha Unyanyasaji na Unyonyaji

Matini inajenga taswira ya dini kama chombo kinachoweza kutumiwa kuwanyonya waumini. Hali hii inaonekana kupitia msisitizo wa zaka, sadaka na michango pamoja na maisha ya baadhi ya viongozi. Dondoo linalohusu sadaka linaonyesha kuwa hata watu wenye hali duni wanatarajiwa kutoa, huku matumizi ya fedha hizo yakizua maswali.

Tukio la mazishi ya Apondi linaendeleza maana hiyo. Badala ya washirika kupunguza mzigo wa familia iliyofiwa, madai ya vifaa na fedha yanaongeza mzigo. Hapa dini inakutana na desturi za kijamii na maslahi ya taasisi, na matini inafichua namna nafasi ya "mtumishi wa Mungu" inaweza kutumiwa katika kudai rasilimali.

> *"Kuanzia Jumapili ijayo, vifuko vya sadaka vitakuwa kule mbele na kila mmoja atapaswa kupeleka zaka yake kila mtu akimwona. Maana kuna watu huja Jumapili mbili hapa wasitoe zaka..." (uk. 54).*

Kauli hii inaonyesha mabadiliko kutoka kutoa kwa hiari kwenda kutoa chini ya shinikizo la kijamii. Hivyo, dhana ya sadaka kama tendo la kiroho inasogezwa karibu na dhana ya wajibu wa kifedha unaosimamiwa na taasisi. Kwa mtazamo wa Udenguzi, maana ya "sadaka" inatetereka kati ya ibada na mfumo wa ukusanyaji wa rasilimali. Mkinzano huo unafungua uwezekano wa kuisoma dini kama huduma na pia kama mfumo unaoweza kuzalisha utegemezi wa kifedha.

Kwa jumla, taswira ya unyonyaji inajengwa pale ambapo matendo ya viongozi na taratibu za taasisi zinapotenganishwa na lengo la huduma kwa waumini.

4.1.8 Dini kama Chanzo cha Maendeleo katika Jamii

Taswira ya mwisho katika kundi hili ni dini kama kichocheo cha maendeleo. Michael anataka Bethany Bible Church iwe taasisi inayowasaidia maskini na kuanzisha miradi kama zahanati na shule. Hivyo, dini inaonyeshwa ikiwa na uwezekano wa kugeuza imani kuwa vitendo vinavyowanufaisha wanajamii.

Taswira hii ni muhimu kwa sababu inakabiliana moja kwa moja na taswira ya dini kama mfumo wa unyonyaji. Katika matini hiyo hiyo, kanisa linaweza kuhusishwa na matumizi mabaya ya fedha, lakini pia linaweza kuhusishwa na miradi ya kijamii. Kwa mtazamo wa Udenguzi, moja haiwezi kufutwa na nyingine; zote mbili zinakuwa sehemu ya maana ya dini katika riwaya.

> *"Michael hakutaka kanisa lake kuwa kama haya mengine. Alitaka kujenga kanisa litakalokuwa mfano katika Kibera nzima kuhusu namna linavyofaa kufanya ibada. Alitaka kanisa litakalosaidia maskini miongoni mwa waumini na kufanya miradi ya kujenga zahanati na skuli za kuwahudumia umma." (uk. 78 na 79).*

Kauli hii inatenganisha huduma ya kweli na kanisa linalojikita katika kujitajirisha. Hata hivyo, maana ya maendeleo hapa inategemea pia tofauti na mifumo ya kidini ambayo riwaya imeikosoa. Kwa hiyo, maendeleo hayajengwi kama maana huru; yanapata uzito kutokana na kile ambacho matini imeonyesha kuwa hakifai.

Kwa hiyo, *Paradiso* inajenga dini kama taasisi yenye uwezo wa kuchochea maendeleo, lakini uwezekano huo unategemea namna huduma, rasilimali na uongozi vinavyotekelezwa.

4.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini katika Riwaya ya *Paradiso*

Sehemu hii inahusu lengo la pili la utafiti, ambalo ni kuchanganua usawiri wa viongozi wa dini katika riwaya teule. Viongozi hawachanganuliwi kwa kuorodhesha sifa zao pekee, bali kwa kuangalia namna sifa hizo zinavyotengenezwa na matendo, kauli, mahusiano na matukio ya matini. Mhimili wa pili wa Udenguzi, unaosisitiza kwamba matini inaweza kuwa na maana mbalimbali zinazokinzana, unatumika kuonyesha kuwa kiongozi mmoja anaweza kujengwa kwa sifa zinazokinzana. Kwa mfano, Michael anaonekana mwaminifu na mwadilifu katika baadhi ya matukio, lakini baadaye anakabiliwa na udhaifu wa kibinadamu. Vilevile, Boribori anaweza kuonekana mwenye bidii katika kuendesha taasisi na wakati huo huo akahusishwa na uhalifu.

Matokeo haya yanaafikiana kwa sehemu na Mosha (2013), ambaye alibaini kuwa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi anaweza kuwa mwelekezi wa jamii na wakati huo huo akaonyeshwa katika matendo kama uzinzi, ulevi na ugomvi. Vilevile, Wanjiru (2022) na Akong'o (2022) wanaonyesha namna uongozi wa kidini unavyoweza kuhusishwa na matumizi mabaya ya mamlaka, tamaa na utajiri. Utafiti huu unaongeza mjadala huo kwa kuonyesha jinsi mikinzano hiyo inavyofanya kazi ndani ya matini moja ya *Paradiso*kwa mtazamo wa Udenguzi.

4.2.1 Viongozi wa Dini kama Waaminifu

Michael anajengwa kama kiongozi mwenye kujitolea katika huduma, hasa kupitia maombi, uinjilisti na utayari wa kuwasaidia waumini. Hata hivyo, uaminifu wake haupaswi kuchukuliwa kama sifa isiyobadilika kwa sababu matini baadaye inamwonyesha akikumbwa na jaribu la uhusiano na Patricia. Hivyo, uaminifu wake unapaswa kuchanganuliwa kama maana inayojengwa kupitia matendo tofauti ya mhusika.

Baada ya kutambua kosa lake, Michael anaomba na kutafuta kurekebisha uhusiano wake na Lydia. Tukio hilo linatoa msingi wa kumwona kama mtu anayekubali uwezekano wa kukosea na kurejea katika misingi anayodai kuifuata.

> *"Aliomba Mungu kwa machozi mazito huku amepiga magoti. Mwili wake wote ulitetemeka akimsihi Mungu na kufanya toba yake..." (uk. 167).*

Uaminifu wa Michael hapa haujengwi na kutokosea. Unajengwa na namna anavyokabiliana na kosa. Hivyo, matini inavuruga upinzani rahisi wa mwaminifu dhidi ya asiye mwaminifu: Michael ni mwaminifu katika huduma, lakini ni dhaifu katika maisha binafsi. Udenguzi unaifanya tofauti hiyo isomwe kama mkondo wa maana unaobadilika badala ya hukumu ya kudumu.

Kwa hiyo, usawiri wa Michael kama mwaminifu unakuwa wa kimkanganyiko kwa sababu uaminifu wake unaonekana pamoja na uwezekano wa kuanguka.

4.2.2 Viongozi wa Dini kama Waadilifu

Uadilifu wa Michael unaonekana katika kukataa malipo ya moja kwa moja baada ya kuwasaidia waumini. Kauli yake kwamba anamfanyia Mungu kazi bure inamtofautisha na viongozi wanaohusishwa na fedha na kujinufaisha.

Tofauti hiyo inajenga mfumo wa kinzani ndani ya matini. Kiongozi mwadilifu anaonekana kwa kuweka huduma mbele ya malipo, lakini uwepo wa viongozi wengine wanaotumia huduma kwa maslahi binafsi unaifanya maana ya uadilifu ionekane kupitia kinyume chake.

> *"Ni za nini hizi pesa?" Michael aliuliza. "Ni chai yako," Amuko alisema. "Hii kazi namfanyia Mungu bure. Tafadhali usinilipe," Michael alisema." (uk. 42).*

Kauli ya Michael inaondoa thamani ya huduma kutoka kwenye malipo ya fedha na kuiweka katika wajibu wa kiroho. Hata hivyo, matini haifanyi uadilifu huu kuwa wa kudumu, kwa sababu baadaye maisha ya Michael binafsi yanamweka katika hali inayopingana na matarajio ya kiongozi mwadilifu. Hivyo, uadilifu unajengwa kama sifa inayoweza kutimia na kutetereka.

Matokeo yanaonyesha kuwa uadilifu wa viongozi katika *Paradiso*unatokana na matendo yao, si cheo chao pekee.

4.2.3 Viongozi wa Dini kama Wavumilivu

Michael anaendelea na huduma yake licha ya mazingira magumu ya Kibera na changamoto za uongozi. Boribori naye anaonyeshwa akivumilia mashaka na upinzani kabla ya kupata nafasi ya kuongoza New Jerusalem.

Hata hivyo, uvumilivu wa Boribori hauwezi kutenganishwa na matukio ya baadaye yanayohusisha uongozi wake. Hivyo, matini inafichua kuwa sifa moja nzuri haiwezi kutabiri tabia yote ya mhusika.

> *"Joshua na James Boribori walikuwa binamu. Mwanzo walipendana lakini baadaye nafasi na harakati zilianza kuwatenganisha. Hata hivyo, Boribori alikuwa mtulivu. Alikaa hapo kanisani akishukiwa, akisutwa." (uk. 198).*

Matini inajenga Boribori kama mtu anayesubiri na kuvumilia. Lakini nafasi anayopata baadaye inafungua maana nyingine ya uvumilivu kwa sababu haimzuii kuhusishwa na matumizi mabaya ya mamlaka. Hivyo, uvumilivu unaonekana kama sifa yenye mipaka, si dhamana ya uadilifu wa baadaye.

Kwa hiyo, uvumilivu ni sehemu ya usawiri wa viongozi, lakini matini inakataa kuufanya kuwa msingi wa hukumu ya mwisho kuhusu mhusika.

4.2.4 Viongozi wa Dini kama Wenye Bidii

Bidii inajitokeza katika shughuli za Boribori, Michael na Nana. Boribori anaendeleza taasisi ya New Jerusalem baada ya kuchukua uongozi, Michael anaendeleza Bethany na mahusiano kati ya viongozi wa makanisa, huku Nana akiendelea na huduma baada ya Boribori kufungwa.

Matini hivyo inahusisha uongozi bora na uwezo wa kuendeleza taasisi. Lakini Udenguzi unatufanya tutenganishe bidii na uadilifu. Boribori anaweza kuwa mwenye bidii katika kuendesha kanisa na wakati huo huo kuhusishwa na matendo yanayokiuka sheria. Hivyo, bidii haisemi yenyewe kwamba mhusika ni mwema.

> *"Michael naye amesimama kidete sasa kama mbuyu. Amekataa kupepesuliwa na upepo wa raha za dunia. Mipangilio yake sasa ni ya kusitawisha kanisa la Bethany." (uk. 225).*

Kauli hii inajenga Michael kama kiongozi anayelenga taasisi na umoja. Hata hivyo, maana hiyo inapata uzito kwa kuwepo kwa viongozi ambao bidii yao inaelekezwa kwenye kujikusanyia mali. Kwa hiyo, matini inatenganisha bidii kama juhudi na matumizi ya juhudi hiyo kama jambo linaloweza kuwa chanya au hasi.

Matokeo yanaonyesha kuwa bidii ni sifa ya utendaji, lakini thamani yake ya kimaadili hutegemea mwelekeo wa matendo ya kiongozi.

4.2.5 Viongozi wa Dini kama Wawajibikaji

Uwajibikaji unaonekana pale ambapo viongozi wanakubali kukabiliana na matendo yao. Michael anapomuomba Lydia msamaha, anachukua hatua ya kukiri kosa lake. Boribori pia, wakati wa kesi yake, anakubali kuwa Michael na baadhi ya viongozi wengine hawakuwa sehemu ya kashfa hiyo.

Kwa mtazamo wa Udenguzi, uwajibikaji hapa una maana inayohusiana na kinyume chake, yaani kutowajibika. Joshua anapomlaumu Michael baada ya mgogoro wa New Jerusalem, matini inatoa mfano wa namna mamlaka inaweza kujaribu kuhamisha lawama. Hivyo, viongozi wanajengwa kati ya kukubali na kukataa wajibu.

> *"Unaonaje sasa?" Michael alimwuliza Lydia. "Uu? Unajisikiaje? Sitarudia kosa hili tena. Limeniletea izara katika marafiki zangu."" (uk. 169).*

Michael anapokiri kosa, anajitokeza kama kiongozi anayekubali kuwa hadhi yake haimfanyi asiwe na makosa. Hii inasumbua wazo la kiongozi kama mtu mkamilifu. Uongozi unakuwa na maana kwa sababu unaambatana na uwezekano wa kukosea na kurekebisha.

Kwa hiyo, uwajibikaji katika *Paradiso* unajengwa kama mchakato wa kukabiliana na kosa, si kama sifa ya kudumu ya viongozi.

4.2.6 Viongozi wa Dini kama Wenye Tamaa na Ubinafsi

Taswira hasi ya viongozi inajitokeza wazi kupitia Tonje, Joshua na Boribori. Tonje anaingia katika ushindani kuhusu washirika na zaka, huku Joshua na Lona wakihusishwa na matumizi ya rasilimali za kanisa kwa maslahi binafsi. Boribori naye baadaye anahusishwa na biashara ya dawa za kulevya.

Utafiti wa Akong'o (2022) ulionyesha kuwa tamaa ya mali na madaraka inaweza kuwafanya viongozi wa dini kuingia katika migogoro, kuwadhulumu waumini na kuvunja misingi ya maadili. Matokeo ya *Paradiso ya*naafikiana na hoja hiyo, lakini yanakwenda zaidi kwa kuonyesha jinsi tamaa inavyobadilisha maana ya huduma yenyewe: huduma inayotarajiwa kuwa ya kiroho inageuka kuwa njia ya kupata mali na mamlaka.

> *"Tonje gani mwanangu? Tonje alifungua kanisa lake mwenyewe. Yeye na babake hawaonani uso kwa uso. Kila mmoja yuko na mambo yake. "Na wanagombea nini?" Michael aliuliza. "Wanagombea washirika na zaka. Pesa zimekuwa uti wa mgongo wa Injili hapa Mombasa."" (uk. 45).*

Maneno "washirika na zaka" yanaweka watu na fedha katika mstari mmoja wa ushindani. Hapo maana ya uongozi wa kidini inatetereka: kiongozi anatakiwa kuwa mlezi wa kiroho, lakini anajengwa pia kama mshindani wa rasilimali. Kwa mujibu wa Udenguzi, maana ya huduma haiwezi kutenganishwa na maana ya biashara inayojitokeza ndani yake.

Kwa hiyo, tamaa na ubinafsi vinakuwa nguzo muhimu za usawiri hasi wa baadhi ya viongozi wa dini katika riwaya.

4.2.7 Viongozi wa Dini kama Wanafiki

Unafiki unajitokeza pale ambapo mwonekano wa nje wa kiongozi unatofautiana na matendo yake. Boribori ni mfano muhimu kwa sababu anaendelea kuonekana kama kiongozi wa kiroho huku

akifahamu udanganyifu unaohusishwa na baadhi ya miujiza na matumizi ya fedha. Mango naye anataka kuabudu bila kufuata kikamilifu baadhi ya kanuni za mfumo wa dini.

Hapa matini inajenga upinzani kati ya ishara ya utakatifu na uhalisia wa matendo. Mhimili wa pili wa Udenguzi unaonyesha kwamba maana ya "kiongozi wa dini" inatetereka pale cheo hicho kinapokutana na vitendo vinavyopingana nacho.

> *"Boribori anakumbuka mkutano aliokuwa nao Kisii mjini. Watu kumi na wanane walishuhudia kupona Ukimwi. Kumbe ni porojo lao la kupanga. Boribori alijuta kufanya hivi... Waumini walimwamini lakini yeye alivachezea shere kwa kuwafanyia tamthilia." (uk. 215).*

Kauli hii inafichua tofauti kati ya kile waumini wanaamini na kile kiongozi anachojua. Hapo ndipo unafiki unapata nguvu ya kifasihi: ishara za ibada zinabaki juu juu, lakini maana yake ya ndani inapingwa na maarifa ya mhusika mwenyewe. Matini hivyo inajenga na kubomoa kwa wakati mmoja taswira ya kiongozi kama mpatanishi wa kweli kati ya Mungu na waumini.

Matokeo yanaonyesha kuwa unafiki unajengwa zaidi kupitia pengo kati ya kauli, nafasi ya kidini na matendo halisi.

4.2.8 Viongozi wa Dini kama Wenye Nguvu za Miujiza

Michael anasawiriwa kama kiongozi mwenye uwezo wa kupokea maono na kuwasaidia watu wanaokumbwa na matatizo. Tukio la Amuko linaonyesha kwamba Michael anadai kupewa ufahamu wa chanzo cha tatizo la mhusika huyo na kumwelekeza kwenye toba.

Hata hivyo, nguvu hizi hazijengwi kama mali binafsi ya Michael. Matini huzihusisha na "roho wa Bwana" na hivyo mamlaka ya kiongozi inategemea chanzo kingine kinachodaiwa kuwa nje yake. Hapa maana ya kiongozi mwenye nguvu inakuwa ya kutegemea uhusiano kati ya mhusika, waumini na imani yao.

> *"Michael aliendelea kuomba huku akipewa maono ya Amuko. Chanzo cha maradhi haya alionyeshwa katika maono." (uk. 40).*

Kauli hii inampa Michael mamlaka ya kutafsiri hali ya Amuko. Lakini kwa Udenguzi, mamlaka hayo hayajitoshelezi yenyewe kwa sababu yanategemea lugha na imani inayotafsiri maono hayo.

Kwa hiyo, kiongozi anakuwa kitovu cha maana kwa muda, lakini chanzo cha mamlaka yake kinabaki katika kile kinachodaiwa kuwa nguvu ya Mungu.

Kwa jumla, nguvu za miujiza zinachangia kumjenga kiongozi wa dini kama mwenye mamlaka ya kiroho, lakini matini haifungi mamlaka hayo katika mtu mwenyewe.

4.2.9 Viongozi wa Dini kama Washauri na Waelekezi

Viongozi wa dini pia wanajengwa kama washauri katika masuala ya ndoa, huduma na mahusiano. Kamati ya New Jerusalem inamshauri Michael kuhusu ndoa, Musa anamwonya kuhusu mahusiano na Lona anasisitiza umuhimu wa kuwafariji waliofiwa.

Hata hivyo, ushauri huu hauwasilishwi kama maana moja ya "uongozi mwema." Ushauri wa Joshua kuhusu watu waliopotoka unatofautiana na msimamo wa Lona wa huruma. Hivyo, viongozi wawili ndani ya taasisi moja wanatoa tafsiri mbili za wajibu wa kidini.

> *"Pole lakini. Maskini amekufa mkewe sijui vipi? Tuende tukamtembelee."*
> *"Sitashirikiana na watenda dhambi mimi," Joshua alisema." (uk. 80).*

Mgongano kati ya Lona na Joshua unaonyesha kuwa uongozi wa kidini hauzalishi sauti moja. Lona anasisitiza huruma, huku Joshua akisisitiza hukumu. Matini hivyo inasambaratisha dhana ya mshauri wa kidini kama mwenye jibu moja linalokubalika kwa wote.

Kwa hiyo, viongozi wa dini kama washauri na waelekezi wanasawiriwa kupitia tofauti za mitazamo yao, jambo linalofanya ushauri wa kidini kuwa eneo la tafsiri na mjadala.

4.2.10 Viongozi wa Dini kama Wenye Udhaifu wa Kibinadamu

Habwe anawajenga viongozi wa dini kama wanadamu wenye udhaifu. Lona anahusishwa na matumizi ya lugha kali na pia tamaa ya kimapenzi, huku Michael akihusishwa na uhusiano na Patricia. Matukio haya yanapinga dhana ya kiongozi wa dini kama mtu aliyejitenga kabisa na udhaifu wa kibinadamu.

Utafiti wa Mosha (2013) ulionyesha pia kwamba kiongozi wa dini katika fasihi anaweza kupewa majukumu ya kiroho huku akionyeshwa katika matendo ya kibinadamu kama uzinzi, ulevi na ugomvi. Matokeo ya *Paradiso i*naendeleza mkondo huo, lakini yanauweka katika mjadala mpana wa maana zinazokinzana za uongozi.

“Habari za Patricia zilimjia tena kwa miezi. Hajui kwa nini. Zilipomjia mwanzo na kumpiga kumbo alipiga magoti akaomba... Fuad yake ilikuwa na hawaa kwa Patricia.” (uk. 150).

Katika dondoo hili, Michael anatambuliwa kama mhubiri anayejua mipaka ya kile anachopaswa kufanya, lakini mawazo na hisia zake zinamvuta upande mwingine. Hivyo, matini inajenga kiongozi kama mwenye maarifa ya kanuni na wakati huo huo mwenye uwezo wa kukiuka kanuni hizo. Udenguzi unafanya mkanganyiko huu kuwa muhimu badala ya kuuondoa ili kutoa hukumu rahisi.

Kwa hiyo, udhaifu wa kibinadamu ni sehemu ya msingi ya usawiri wa viongozi wa dini katika *Paradiso* na unaifanya taswira yao isiwe ya ukamilifu usio na dosari.

4.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii katika Riwaya ya *Paradiso*

Sehemu hii inatekeleza lengo la tatu la utafiti kwa kubainisha namna dini inavyohusishwa na mabadiliko ya maadili ya jamii katika *Paradiso*. Uchanganuzi hauchukulii dini kuwa chanzo cha maadili kwa upande mmoja tu. Badala yake, matini inaonyesha athari chanya na hasi. Mhimili wa tatu wa Udenguzi, unaoangalia maana katika hali ya kuwepo na kutokuwepo, unafaa katika sehemu hii kwa sababu maadili yanayohusishwa na dini yanaonekana pamoja na vitendo vinavyoyapinga. Upendo unaweza kuonekana pamoja na chuki, msamaha pamoja na usaliti, uwajibikaji pamoja na ubinafsi, na umoja pamoja na migawanyiko.

Matokeo haya yanaendana kwa sehemu na mjadala wa Mugha (1999), Magare (2002), Cooper (2004), Mose (2005), Mbatiah (2008), Ogutu (2013), Matundura (2019) na Abdallah (2021), ambao katika mapitio ya maandishi walionyesha namna kazi za fasihi zinavyohusisha dini, imani, utamaushi, migogoro na hali ya maisha ya jamii. Hata hivyo, uchanganuzi wa sasa unaweka mkazo mahsusi kwenye namna matini ya *Paradiso*inavyojenga na kubomoa maana za maadili kupitia matendo ya wahusika na taasisi za dini.

4.3.1 Athari Chanya

Katika upande chanya, dini inahusishwa na umoja, kupunguza vitendo viovu, kusaidiana, msamaha na uwajibikaji. Hoja hizi hazichukuliwi kama ukweli wa jumla kuhusu dini, bali kama maana ambazo matini inazijenga kupitia matukio na wahusika.

4.3.1.1 Dini Imeleta Umoja Baina ya Wanajamii

Mikutano ya kidini na shughuli za uinjilisti za Michael zinawaleta pamoja watu kutoka maeneo na makundi mbalimbali. Mkutano wake wa Mombasa na baadaye mikutano inayohusisha viongozi wa dini mbalimbali inaonyesha uwezekano wa dini kuwa nafasi ya kukutana na kusikilizana.

Hata hivyo, maana ya umoja hapa inajengwa pamoja na kumbukumbu ya migawanyiko ya makanisa. Kwa hiyo, umoja unaonekana kuwa jambo linalohitaji kujengwa upya, si hali ya kudumu inayotokana moja kwa moja na uwepo wa dini.

> *"Tunaishi katika dunia moja kwa hivyo licha ya kuwa na tofauti hizo zote lazima tutafute mwafaka wa kusikilizana, kusaidiana na kuelekezana," Michael alieleza." (uk. 228).*

Kauli ya Michael inapanua umoja kutoka kundi moja la waumini hadi watu wa dini tofauti. Kwa mtazamo wa Udenguzi, neno "tofauti" lina umuhimu kwa sababu umoja hauondoi tofauti; unajengwa kwa kukubali kuwepo kwake. Hivyo, umoja wa kidini katika matini haujengwi kama kufutwa kwa tofauti, bali kama uwezekano wa kuishi pamoja licha ya tofauti.

Kwa hiyo, dini inaonyeshwa kuwa na uwezo wa kuleta umoja, lakini umoja huo unategemea namna tofauti zinavyotafsiriwa na kushughulikiwa.

4.3.1.2 Dini Imepunguza Vitendo Viovu katika Jamii

Mahubiri ya Michael yanakemea uzinzi, uovu na tabia zinazokiuka misingi ya maadili. Aidha, masharti ya kanisa kuhusu ulevi, kimada na ndoa yanaweka mipaka ya kitabia kwa waumini.

Hata hivyo, matini yenyewe inatoa swali kuhusu uthabiti wa mipaka hiyo. Mango anahoji tofauti kati ya masharti ya kanisa na mifano ya wahusika wa Biblia kuhusu wake wengi. Hivyo, kanuni inayokusudiwa kudhibiti uovu inaweza yenyewe kuibua mjadala kuhusu msingi wake.

> *"Kwa nini mnaona ajabu? Leo mtu kulala na binti yake si jambo kubwa!... Lazima turekebishe tabia na mienendo yetu ikiwa tutaendelea kumhubiria Bwana na kumfanyia kazi..." (uk. 56).*

Mahubiri haya yanajenga dini kama sauti ya kukemea uovu. Lakini matini pia inawaonyesha baadhi ya wahubiri wakikiuka misingi wanayoihubiri. Kwa hiyo, athari ya dini katika kupunguza uovu inategemea utekelezaji wake. Hapo ndipo mhimili wa tatu wa Udenguzi unapotumika: maana

ya “maadili ya kidini” ipo katika mafundisho na pia katika kutokuwepo kwake kwenye matendo ya baadhi ya wahusika.

Kwa jumla, dini inaonekana kuwa na uwezo wa kudhibiti baadhi ya mienendo, lakini matokeo hayo hayajajengwa kama ya kudumu kwa sababu matini inatoa mifano ya ukiukaji.

4.3.1.3 Dini Imehimiza Kusaidiana kati ya Watu

Ushauri wa Michael kwa Agripina na ushiriki wa waumini katika harusi na matukio mengine unaonyesha dini kama chanzo cha msaada wa kijamii na kihisia. Michael anamsikiliza Agripina na kumhimiza kuwa na subira, huku shughuli za kanisa zikijenga mitandao ya watu wanaosaidiana.

Matini pia inaonyesha msaada kama jambo linalotokea kupitia mahusiano ya waumini, si kwa mahubiri pekee. Hivyo, dini inakuwa nafasi ya kujenga uhusiano wa kijamii unaoweza kusaidia mtu katika kipindi cha matatizo.

> *“Vumilia, Mungu atajibu maombi yako. Mungu ndiye aumbaye na kuumbua,” Michael alimweleza.” (uk. 99).*

Kauli hii inaonyesha kuwa ushauri wa kidini unamwondoa Agripina kutoka katika kumlaumu mumewe na kumwelekeza kwenye subira. Hata hivyo, matini haionyeshi kwamba msaada huo unaondoa matatizo yote. Maana ya kusaidiana inabaki kuwa katika mchakato wa kupeana faraja na mwongozo.

Kwa hiyo, dini inajengwa kama mtandao wa msaada wa kijamii, hasa kupitia mahusiano kati ya waumini na viongozi.

4.3.1.4 Dini Imeimarisha Msamaha kati ya Watu

Msamaha ni mojawapo ya maadili yanayoonekana wazi katika uhusiano wa Lydia na Michael. Baada ya Michael kukosea, Lydia anamwambia amemsamehe. Tukio hilo linaonyesha dini ikiathiri maamuzi ya mtu kwa kumwelekeza kutoka kulipiza kisasi kwenda kusamehe.

Hata hivyo, msamaha hauondoi kosa lililotangulia. Kinyume chake, uwepo wa kosa ndio unaofanya msamaha uwe na maana. Hivyo, kwa mtazamo wa Udenguzi, msamaha unajengwa pamoja na usaliti na maumivu yaliyoutangulia.

> *“Nimekusamehe Michael,” Lydia alisema hatimaye. “Asante Lydia,” Michael alisema huku akikaza mkono wake kwenye ule wa Lydia.” (uk. 170).*

Msamaha wa Lydia unavunja mnyororo wa kosa na kulipiza kisasi. Lakini pia unakumbusha kuwa maadili ya msamaha yanakuwa na maana kwa sababu kuna kosa linalohitaji kusamehewa. Hivyo, matini inajenga msamaha na kosa kama maana zinazotegemeana.

Kwa hiyo, dini inaonekana kuchangia maadili ya msamaha, lakini msamaha wenyewe hauwezi kutenganishwa na uwepo wa migogoro na makosa.

4.3.1.5 Dini Imekuza Uwajibikaji Miongoni mwa Watu

Amuko anakubali kuhusishwa na kafara na kutafuta msamaha. Salome anaomba msamaha kwa mumewe na kwa waumini, huku Michael akikiri kosa lake mbele ya Lydia. Matukio haya yanaonyesha dini ikitengeneza mazingira ya kukiri kosa na kutafuta marekebisho.

Hata hivyo, uwajibikaji haujitokezi kwa wahusika wote kwa kiwango sawa. Tofauti kati ya wanaokiri makosa na wanaojitetea inafanya uwajibikaji uwe sehemu ya mvutano wa kimaadili katika matini.

> *""Utanisamehe Kyalo?" Salome aliuliza. "Sitakusamehe." Kyalo alisema. "Kwa nini, daddy?" "Kwa sababu nilikusamehe usiku ule."" (uk. 59).*

Mazungumzo haya yanaonyesha kwamba msamaha na uwajibikaji vinaingiliana. Salome anakiri kosa, huku Kyalo akikumbusha kuwa msamaha ulikuwa tayari umetolewa. Hivyo, uwajibikaji unakuwa sehemu ya mchakato wa kurejesha uhusiano.

Kwa hiyo, dini katika matukio haya inaonekana kuchochea uwajibikaji, hasa pale mhusika anapokubali kukabiliana na matendo yake.

4.3.2 Athari Hasi

Katika upande hasi, dini inahusishwa na migogoro, chuki, tamaa na ubinafsi, misimamo mikali na unafiki. Hapa pia mtafiti haichukulii dini yenyewe kama chanzo cha moja kwa moja cha maovu yote. Uchambuzi unaangalia namna matini inavyoweka taasisi ya dini, viongozi, waumini na maslahi yao katika mahusiano yanayozalisha matokeo hayo.

4.3.2.1 Dini Imeleta Migogoro na Migawanyiko

Mgogoro wa New Jerusalem unaonyesha wazi namna mashindano ya uongozi yanavyoweza kugawanya waumini. Tofauti kati ya Joshua na Michael inapanuka hadi kuwa mapambano ya vikundi. Waumini ambao hapo awali waliitwa ndugu wanajikuta katika makundi yanayopingana.

Hapa dini inabaki kuwa mazingira ya migogoro, lakini chanzo cha mgogoro kinaonekana katika tamaa ya mamlaka na ushindani wa viongozi. Hivyo, matini inatenganisha taasisi na matumizi yake: dini inaweza kuwa jina la taasisi, huku maslahi ya binadamu yakitawala matendo yake.

> *"Baadaye walifikia uamuzi wa kuvunja kanisa la New Jerusalem. Michael alihuzunika. Aliona kanisa la Bwana likisambaratika kila siku, kila mwezi, kila mwaka." (uk. 77).*

Kauli hii inafichua kinzani kati ya jina la "kanisa la Bwana" na hali ya kusambaratika kwake. Kanisa linapaswa kuashiria umoja, lakini matini inalionyesha likivunjwa na watu wanaojiita ndugu. Huu ndio mkinzano unaotumiwa na Udenguzi kufichua kutotulia kwa maana ya taasisi ya kidini.

Kwa hiyo, dini katika matukio haya inahusishwa na migawanyiko, hasa pale mamlaka ya kidini inapochanganywa na ushindani wa kibinadamu.

4.3.2.2 Dini Imesababisha Chuki Baina ya Waumini

Wivu na chuki dhidi ya Michael zinajitokeza anapopata umaarufu katika huduma. Joshua na Monayo wanatilia shaka uwezo wake na kutabiri kushindwa kwake. Chuki hiyo baadaye inaambatana na migogoro mikubwa zaidi.

Sakina anaeleza kwa uwazi kuwa kuna matukio ya kutiliana sumu na kashfa ndani ya mazingira yanayohusishwa na dini. Hapa matini inajenga upendo kama matarajio ya dini na chuki kama uhalisia unaojitokeza. Upinzani huo ndio unaofanya athari ya dini katika maadili ionekane kuwa ya pande mbili.

> *""Dini zenu hizo mwanangu zina matatizo. Kutiliana sumu, mara kutongozana. Kashifa zimezidi." "Ni kweli. Lakini si dini ni ulimwengu ulivyo," Michael alisema." (uk. 63).*

Jibu la Michael ni muhimu kwa sababu halikubali moja kwa moja kwamba dini yenyewe ndiyo chanzo cha matatizo. Sakina anaunganisha matatizo na dini, lakini Michael anayahamisha kwenye "ulimwengu ulivyo." Matini kwa hiyo inatoa tafsiri mbili zinazokinzana kuhusu chanzo cha uovu. Hii ni mifano ya wazi ya maana isiyotulia ambayo mhimili wa tatu wa Udenguzi unaruhusu kuchanganuliwa.

Kwa hiyo, chuki inahusishwa na mazingira ya kidini, lakini matini inaacha wazi iwapo dini yenyewe au hali ya kibinadamu ndiyo chanzo kikuu.

4.3.2.3 Dini Imechochea Tamaa na Ubinafsi Miongoni mwa Viongozi

Matendo ya Joshua, Lona na Boribori yanaonyesha namna rasilimali za kanisa zinavyoweza kugeuzwa kuwa chanzo cha kujinufaisha. Fedha zinazotolewa kwa ajili ya kanisa zinaelekezwa katika akaunti za viongozi, huku Boribori baadaye akihusishwa na biashara ya dawa za kulevya.

Matokeo haya yanaafikiana na Muli (2024), ambaye katika mapitio ya maandishi alibainisha matumizi ya dini kama njia ya kujitajirisha na uwepo wa biashara haramu zinazohusishwa na taasisi za kidini. Katika *Paradiso*, matini inafanya suala hilo kuwa sehemu ya ujenzi wa maadili: kiongozi anayepaswa kuwa mfano anakuwa mhusika anayekiuka misingi hiyo.

> *"Viongozi walipiga magoti kwenye madhabahu, wakatiliwa mikono na watukufu wa Bwana. Kama ilivyokuwa desturi walichanga pesa kwa miradi ya kanisa la New Jerusalem. Askofu Joshua na kasisi Lona Bosire walipokea misaada yote wakaiweka katika akaunti zao kwa niaba ya kanisa la New Jerusalem." (uk. 130).*

Kitendo cha kupokea fedha kwa jina la kanisa na kuziweka katika akaunti binafsi kinavuruga mpaka kati ya mali ya taasisi na mali ya kiongozi. Kwa hiyo, matini inajenga tamaa kama tatizo la kimaadili linalotokana na kuvunjika kwa mpaka huo. Hapa dini inabaki katika maneno ya ibada, lakini matendo yanaelekea kwenye maslahi binafsi.

Kwa hiyo, tamaa na ubinafsi vinaonekana kama athari hasi zinazoweza kutokea pale mamlaka ya kidini inapowekwa chini ya maslahi binafsi.

4.3.2.4 Dini Imechochea Msimamo Mkali

Msimamo mkali unaonekana pale waumini wanapowaunga mkono viongozi wao hata baada ya viongozi hao kutiwa hatiani. Baadhi yao wako tayari kufungwa pamoja na viongozi wao. Hali hii inaonyesha uaminifu wa kundi unaoweza kupunguza uwezo wa mtu kuhoji matendo ya kiongozi.

Kwa mtazamo wa Udenguzi, tukio hili linaonyesha mgongano kati ya imani na uwezo wa kuchunguza. Imani inapaswa kuhusishwa na maadili na ukweli, lakini matini inaonyesha hali ambayo imani ya kundi inaweza kutumika kupinga uwajibikaji.

> *"Waumini walikuwa tayari kufungwa na mkubwa wao." (uk. 218).*

Kauli hii ni fupi lakini ina uzito kwa sababu inaonyesha namna utii kwa kiongozi unavyoweza kuzidi uamuzi wa mtu binafsi. "Mkubwa" anakuwa kitovu cha maana kwa waumini, lakini tukio

la hukumu linaufanya utii huo uonekane kuwa na utata. Hivyo, matini inafichua upande wa pili wa uaminifu wa kidini: unaweza kuwa mshikamano, lakini pia unaweza kuzuia ukosoaji.

Kwa hiyo, msimamo mkali unajengwa kama athari hasi pale utii wa kidini unapogeuka kuwa kukubali bila kuhoji.

4.3.2.5 Dini Imechangia Unafiki Miongoni mwa Waumini

Unahusishwa na pengo kati ya mwonekano wa ibada na matendo halisi. Boribori anaendelea kushiriki katika maombi huku akiwa na maarifa kuhusu udanganyifu unaohusishwa na baadhi ya matendo yake. Lona naye anahusishwa na vitendo visivyolingana na utambulisho wake wa kidini.

Tukio hili linaonyesha kuwa ibada ya nje haiwezi kuwa ushahidi wa moja kwa moja wa maadili ya ndani. Kwa mtazamo wa Udenguzi, maana ya "mcha Mungu" inajengwa pamoja na "mnafiki" kwa sababu matini inaonyesha ishara za utauwa zikiwa sambamba na matendo yanayopingana nazo.

> *"Boribori na waumini wake walienda katika uwanja wa Uhuru Park. Walisoma Biblia na kuswali kwa muda wa saa moja. Ilikuwa dhahiri Mungu alisikia sala yao jinsi walivyoomba kwa makenge na kuinua mikono." (uk. 217).*

Ushahidi huu wa ibada unakuwa wa utata unapowekwa karibu na matukio yanayomhusisha Boribori na uhalifu. Hivyo, matini inasababisha msomaji kujiuliza kama ibada ya nje inaweza kuwakilisha mabadiliko ya ndani. Mkinzano huo ndio unaoifanya unafiki kuwa suala la kimaadili, si tu tabia ya mtu mmoja.

Kwa jumla, matini inajenga unafiki kama athari hasi inayojitokeza pale ishara za kidini zinapotenganishwa na matendo.

4.4 Hitimisho

Kwa jumla, sura hii imechanganua data ya utafiti kwa kuzingatia malengo matatu na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi iliyoteuliwa. Katika lengo la kwanza, uchanganuzi umeonyesha kuwa taswira ya dini katika *Paradiso* ni ya pande nyingi, ambapo dini inajengwa kama chanzo cha tumaini, wokovu, miujiza, wito na maendeleo, lakini pia kama mazingira ya migogoro, kanuni kali na unyonyaji. Kwa kuzingatia mhimili wa kwanza, hakuna taswira moja inayoweza kuchukuliwa kuwa maana ya mwisho ya dini kwa kuwa maana hizo hujitokeza kupitia uhusiano na mikinzano

yake ndani ya matini. Katika lengo la pili, uchanganuzi umeonyesha kuwa viongozi wa dini wamesawiriwa kwa sifa zinazokinzana. Michael anaonekana mwaminifu, mwadilifu, mvumilivu na mwenye bidii, lakini pia ana udhaifu wa kibinadamu, huku Boribori akionyeshwa kama kiongozi mwenye bidii na mvumilivu ambaye baadaye anahusishwa na tamaa, unafiki na uhalifu. Lona, Joshua na viongozi wengine pia wanaoneshwa kupitia mchanganyiko wa sifa chanya na hasi, jambo linaloonyesha kuwa cheo cha kidini hakiwezi kutoa maana moja ya mwisho kuhusu mhusika. Katika lengo la tatu, matokeo yameonyesha kuwa dini ina athari chanya na hasi katika maadili ya jamii, kwa kuwa inaweza kuhimiza umoja, msamaha, kusaidiana na uwajibikaji, lakini pia kuhusishwa na migogoro, chuki, tamaa, misimamo mikali na unafiki. Kwa msingi wa mhimili wa tatu, maana ya maadili haya hujitokeza kupitia uhusiano kati ya kile kinachokuwepo na kile kinachopingwa katika matini. Kwa jumla, data inaonyesha kuwa *Paradiso* inajenga na wakati huo huo kuyumbisha maana kuhusu dini, viongozi wake na nafasi yake katika maadili ya jamii.

SURA YA TANO
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu, muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Kwanza, inaeleza kwa muhtasari mwelekeo wa utafiti kuanzia mada, tatizo la utafiti, malengo, nadharia na mbinu zilizotumika. Pili, inawasilisha kwa ufupi matokeo yaliyopatikana kwa kuzingatia malengo matatu ya utafiti. Tatu, inatoa hitimisho linalotokana na matokeo hayo na kuonyesha mchango wa utafiti katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili na matumizi ya Nadharia ya Udenguzi. Mwisho, inatoa mapendekezo ya kijumla pamoja na maeneo ya utafiti wa baadaye.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umechunguza taswira ya dini katika riwaya ya *Paradiso* John Habwe. Utafiti ulilenga kuchanganua namna dini inavyosawiriwa katika matini, namna viongozi wa dini wanavyowasilishwa, na athari za dini katika maadili ya jamii. Msukumo wa utafiti ulitokana na umuhimu wa dini kama kipengele cha maisha ya jamii na namna fasihi inavyoweza kuijenga, kuikosoa na kuibainisha kupitia wahusika, matukio na mahusiano yao.

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Udenguzi, inayosisitiza kuwa maana ya matini si thabiti na inaweza kujitokeza kwa namna nyingi, ikiwamo kupitia mikinzano ya ndani ya matini. Mihimili mitatu iliteuliwa na kutumika katika uchanganuzi: hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi; matini ya fasihi huwa na maana mbalimbali zinazokinzana; na maana haipatikani katika ishara moja pekee bali hujengwa kupitia hali ya kuwepo na kutokuwepo. Mihimili hii ilitumika kuichunguza dini, viongozi wake na athari zake katika maadili bila kuichukulia taswira yoyote kama maana ya mwisho ya matini.

Utafiti ulitumia muundo wa utafiti wa kimaelezo. Riwaya ya *Paradiso* iliteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia namna inavyoshughulikia masuala ya dini, viongozi wa dini na maisha ya jamii. Data ilikusanywa kwa kusoma matini kwa makini, kubainisha dondoo zinazohusiana na malengo ya utafiti, kuzirekodi na kuzipanga kwa mada. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Udenguzi.

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inawasilisha kwa ufupi matokeo makuu ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Muhtasari huu haujirudii kama maelezo ya sura ya nne, bali unaunganisha hoja kuu zilizojitokeza kutokana na uchanganuzi.

5.3.1 Taswira ya Dini katika Riwaya Teule

Utafiti umebaini kuwa dini katika *Paradiso* imejengwa kwa taswira zinazotofautiana na wakati mwingine kukinzana. Kwa upande mmoja, dini inasawiriwa kama chanzo cha tumaini, njia ya wokovu, chanzo cha miujiza na uponyaji, na wito wa mtu wa kujitolea katika huduma ya Mungu. Taswira hizi zinaonekana kupitia wahusika kama Michael, Mango, Salome, Musa na Amuko. Kwa upande mwingine, dini inajengwa kama chanzo cha migogoro na utengano, mfumo wenye kanuni kali, pamoja na chombo kinachoweza kutumiwa kwa unyanyasaji na unyonyaji. Kwa mtazamo wa Udenguzi, mkinzano huu unaonyesha kuwa taswira ya dini katika matini haiishii katika maana moja, bali inajengwa upya kulingana na matukio, wahusika na mitazamo inayojitokeza katika matini.

5.3.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini katika Riwaya Teule

Matokeo yanaonyesha kuwa viongozi wa dini wamesawiriwa kwa namna changamano. Baadhi yao, hasa Michael, wanajitokeza kama waaminifu, waadilifu, wavumilivu, wenye bidii, wawajibikaji, washauri na waelekezi. Hata hivyo, matini pia inawajenga baadhi ya viongozi kama wenye tamaa na ubinafsi, wanafiki na wenye udhaifu wa kibinadamu. Joshua na Boribori ni mifano ya viongozi ambao matendo yao yanakinzana na matarajio ya uongozi wa kidini. Mkinzano huu unadengua dhana ya kiongozi wa dini kama mhusika mwenye sifa moja isiyobadilika na kuonyesha kuwa usawiri wake unategemea matendo na mahusiano yanayojengwa katika matini.

5.3.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii katika Riwaya Teule

Utafiti umebaini kuwa dini ina athari chanya na hasi katika maadili ya jamii kama yanavyosawiriwa katika *Paradiso*. Kwa upande chanya, dini inahusishwa na umoja, kusaidiana, msamaha na uwajibikaji, pamoja na kupunguza baadhi ya vitendo viovu. Kwa upande hasi, inahusishwa na migogoro, migawanyiko, chuki, tamaa, ubinafsi, misimamo mikali na unafiki. Kwa mujibu wa Udenguzi, mkinzano huu unaonyesha kuwa uhusiano kati ya dini na maadili

hauwezi kufungwa katika tathmini ya upande mmoja. Maana ya mchango wa dini hujitokeza kupitia mvutano kati ya maadili yanayodaiwa na matendo yanayoonekana katika matini.

5.4 Hitimisho

Kwa jumla, utafiti huu unahitimisha kuwa *Paradiso*inajenga taswira ya dini isiyo na maana moja ya mwisho. Matini inaiwasilisha dini kwa sura zinazokinzana, ambapo inajitokeza wakati mmoja kama chanzo cha tumaini, wokovu na mshikamano, na wakati mwingine kama eneo la migogoro, unyonyaji na ukandamizaji. Hivyo, matini inamwezesha msomaji kuona dini kupitia mitazamo mbalimbali badala ya kuipokea kama dhana yenye maana iliyofungwa.

5.4.1 Taswira ya Dini

Kuhusu lengo la kwanza, utafiti unahitimisha kuwa taswira ya dini katika *Paradiso* inajengwa kupitia mikinzano kati ya taswira chanya na hasi. Dini huonekana kuwa na uwezo wa kutoa tumaini, wokovu na mwelekeo wa maisha, lakini pia huweza kuhusishwa na migogoro na matumizi mabaya ya mamlaka. Kwa mtazamo wa mhimili wa kutokuwepo kwa toleo la mwisho la kazi ya fasihi, taswira hizi haziwezi kufungwa katika tafsiri moja pekee. Mchango wa utafiti hapa ni kuonyesha namna matini ya Kiswahili inavyoweza kudenguliwa ili kufichua maana zinazoshindana kuhusu taasisi ya dini.

5.4.2 Usawiri wa Viongozi wa Dini

Kuhusu lengo la pili, utafiti unahitimisha kuwa viongozi wa dini katika *Paradiso* hawasawiriwi kwa namna ya aina moja. Michael anajitokeza kwa sifa chanya, ilhali Joshua, Boribori na Lona wanaonyesha kwa viwango tofauti mivutano kati ya wajibu wa kidini na udhaifu wa kibinadamu. Kwa kutumia mhimili wa maana mbalimbali zinazokinzana, utafiti unaonyesha kuwa matini inajenga na wakati huohuo inavuruga matarajio ya kawaida kuhusu kiongozi wa dini. Hivyo, utafiti unaongeza uelewa wa namna usawiri wa wahusika wa kidini unavyoweza kuchanganuliwa kwa mtazamo wa Udenguzi.

5.4.3 Athari za Dini katika Maadili ya Jamii

Kuhusu lengo la tatu, utafiti unahitimisha kuwa athari za dini katika maadili ya jamii zinajitokeza kwa namna mbili zinazokinzana. Dini inahusishwa na mshikamano, msamaha, kusaidiana na uwajibikaji, lakini pia inahusishwa na migogoro, chuki, tamaa, misimamo mikali na unafiki. Mhimili unaoeleza kuwa maana haipatikani katika ishara moja pekee unaonyesha kuwa maana ya mchango wa dini hujengwa katika uhusiano kati ya madai ya imani na matendo ya wahusika. Kwa

hiyo, utafiti unaonyesha uwezekano wa kutumia Udenguzi kuchanganua mikinzano ya kimaadili ndani ya matini ya fasihi.

5.4.4 Mchango wa Nadharia ya Udenguzi

Kwa upande wa kinadharia, utafiti umeonyesha kuwa Nadharia ya Udenguzi inafaa katika kuchanganua taswira ya dini kwa sababu inamwezesha mtafiti kuchunguza maana zinazokinzana ndani ya matini badala ya kutafuta maana moja ya mwisho. Mihimili iliyoteuliwa imewezesha kuhusisha taswira ya dini, usawiri wa viongozi wa dini na athari za dini katika maadili ya jamii na kufichua mikinzano inayojengwa na matini. Kwa upande wa kifasihi, utafiti umeonyesha namna *Paradiso*inavyotumia wahusika na matukio ya kidini kujenga maana zinazobadilika na zinazoweza kusomwa kwa mitazamo tofauti.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Mapendekezo ya utafiti yamegawanywa katika mapendekezo ya kijumla yanayotokana na matokeo ya utafiti huu na mapendekezo kwa utafiti wa baadaye.

5.5.1 Mapendekezo ya Kijumla

Wataalamu na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili wazidi kuzingatia namna matini zinavyowasilisha dini kwa mitazamo inayokinzana badala ya kuichukulia dini kwa mtazamo mmoja.

Wahakiki wa fasihi wazidi kutumia nadharia zinazofaa katika kuchanganua maana zinazojengwa na kuvunjwa ndani ya matini za kifasihi, hususan katika masuala yanayohusu dini, mamlaka na maadili.

Wasomaji wa fasihi ya Kiswahili wahimizwe kusoma matini za kidini kwa mtazamo wa kiuchanganuzi unaotambua tofauti kati ya mafundisho yanayowasilishwa na matendo ya wahusika.

5.5.2 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye

Utafiti wa baadaye unaweza kuchunguza taswira ya dini katika riwaya nyingine za Kiswahili ili kulinganisha mikinzano inayojitokeza katika *Paradiso* na matini nyingine, pamoja na kuchunguza mabadiliko ya usawiri wa viongozi wa dini katika kazi za waandishi mbalimbali na vipindi tofauti. Aidha, tafiti zinaweza kuchanganua uhusiano kati ya dini na maadili ya jamii katika mazingira mbalimbali ya kijamii, pamoja na mapokezi ya wasomaji kuhusu taswira ya dini, viongozi wa dini na mikinzano ya kimaana katika matini za Kiswahili. Utafiti mwingine unaweza kuchunguza

nafasi ya wanawake katika uongozi wa kidini katika fasihi ya Kiswahili, hasa namna wahusika wa kike wanavyojenga, kuendeleza au kupinga mamlaka ya kidini. Vilevile, tafiti zijazo zinaweza kutumia Nadharia ya Udenguzi kuchanganua maudhui mengine yanayohusiana na dini katika fasihi ya Kiswahili ili kupanua matumizi na uelewa wa nadharia hiyo katika uhakiki wa kifasihi.

MAREJELEO

Agboadanno, K. A. D., & Dossouou, A. M. (2018). Fake prophets and evangile for sale in Amma Darko's *Not without flowers*. *International Journal on Studies in English Language and Literature, 6*(6), 15–29. https://doi.org/10.20431/2347-3134.0606003

Akong'o, T. O. (2022). *Tamaa na athari zake katika jamii: Ulinganishi wa Ua la Faraja na Paradiso* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/163192

Atieno, J. (2019). *Utambulisho wa jinsia katika Maumbile si Huja na Paradiso* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/160768

Best, J. W., & Kahn, J. V. (2009). *Research in education* (10th ed.). PHI Learning.

Browning, D. S., & Cooper, T. D. (2004). *Religious thought and the modern psychologies* (2nd ed.). Fortress Press.

Chimerah, A. M. (2021). *Udhanaishi katika riwaya za Thomas Kamugisha: Kitu Kidogo Tu! na Harusi ya Wendawazimu* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Pwani]. Pwani University Institutional Repository. https://elibrary.pu.ac.ke/handle/123456789/1072

Derrida, J. (1967). *De la grammatologie*. Les Éditions de Minuit.

Durkheim, É. (1912). *Les formes élémentaires de la vie religieuse: Le système totémique en Australie*. Alcan.

Eliade, M. (1957). *The sacred and the profane: The nature of religion*. Harcourt, Brace & World.

Freud, S. (1927). *The future of an illusion*. Hogarth Press.

Golafshani, N. (2003). Understanding reliability and validity in qualitative research. *The Qualitative Report, 8*(4), 597–607. https://doi.org/10.46743/2160-3715/2003.1870

Habwe, J. (2005). *Paradiso*. Jomo Kenyatta Foundation.

Ikunga, S. A., & Abiobio, P. H. (2018). The challenging contemporary issues against church growth in Nigeria: Implication on poor discipleship: A diplomatic historical imperative. *International Journal of Humanities, Social Sciences and Workplace Ergonomics in Africa, 11*(6), 23–32.

Jesse, M. J., King'ei, G. K., & Wafula, R. M. (2019). *Uhusiano wa historia na itikadi katika riwaya teule za S. A. Mohamed*. Chalufakita. http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/22239

Karanja, E. W. (2005). *Nafasi ya dini katika jamii ya kisasa kama ilivyosawiriwa katika riwaya za Nguvu ya Sala, Walenisi na Babu Alipofufuka* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/155580

Kombo, D. K., & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International.

Kumar, R. (2011). *Research methodology: A step-by-step guide for beginners* (3rd ed.). SAGE.

Magare, W. A. (2002). *Uhakiki wa tamthilia ya Amezidi kama kazi ya kiubwege* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Marx, K. (1844). A contribution to the critique of Hegel's philosophy of right: Introduction. *Deutsch-Französische Jahrbücher*.

Matundura, B. (2019, June 12). Kauli ya Matundura: Mchango wa fasihi ya Kiswahili katika kuhifadhi matukio muhimu ya historia. *Taifa Leo*.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya fasihi*. Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbiti, J. S. (1969). *African religions and philosophy*. Heinemann.

Mose, E. N. (2005). *Taashira za kifo katika tamthilia za Mukwava wa Uhehe, Amezidi, Kilio cha Haki na Visiki* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/2184

Mosha, P. G. (2013). *Usawiri wa mhusika Padri katika riwaya za Kezilahabi: Uchanganuzi katika Rosa Mistika, Gamba la Nyoka na Nagona* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam].

Muli, S. M. (2024). *Athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana katika riwaya teule za Paradiso na Kidagaa Kimemwozea* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Mount Kenya University]. Mount Kenya University Repository. https://erepository.mku.ac.ke/handle/123456789/7011

Mungah, C. I. (1999). *Dhana ya maisha katika novela mbili za Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/123456789/21045

Murithi, M. M. (2015). *Uchanganuzi wa methali za Kiswahili: Mtazamo wa kiudenguzi* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository.

Muslim Council of Elders. (2024, September 21). *Secretary-General of the Muslim Council of Elders emphasizes the importance of strengthening the role of religions in shaping the future and addressing global challenges*. https://www.muslim-elders.com/Home/MediaCenterDetail/10445?lang=en

Ng'etich, K. D. (2011). *Dini kama chombo cha kuwadhulumu waumini: Mifano kutoka fasihi katika Kiswahili* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Kenyatta University]. Kenyatta University Institutional Repository. http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/19495

Njenga, A. W. (2021). *Uongozi unavyojitokeza katika fasihi ya kisasa: Uchunguzi wa riwaya mpya ya miaka ya 2000* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Moi].

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Nyandiri, O. C. (2020). Christianity at crossroad: Contemporary challenges facing mainstream church leadership in Kenya. *International Multilingual Journal of Science and Technology, 5*(9).

Ogutu, O. G. (2013). *Athari za Sheng katika dini ya Kikristo: Mtaa wa Umoja* [Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Oko, A. E., & Umanah, A. E. (2022). Proliferation of churches in Nigeria and its impact on national development. *Journal of Philosophy, Culture and Religion, 28*.

Osajie, J. N. (2021). Religious leaders as agents of peace and security for sustainable development in Nigeria. *UJAH: Unizik Journal of Arts and Humanities, 21*(3), 260–273. https://doi.org/10.4314/ujah.v21i3.1572

Princewell, A. N. (2017). Church commercialization in Nigeria: Implications for public relations practice. *Journal of Philosophy, Culture and Religion, 28*, 1–11.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.

Zuhri, M. M., Rokhman, F., Nuryatin, A., & Raharjo, T. J. (2021). Community development: The role of religious leaders in community empowerment. *IOSR Journal of Humanities and Social Science, 26*(11), 37–41. https://doi.org/10.9790/0837-2611073741

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I: Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki

THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

AMECEA

22/09/25

To whom it may concern

RE: OCHARO FRANCINE MA/KIS/ 1051146

It is our pleasure to inform you that Francine Ocharo is a student in our Department of Languages, Literature and Communication undertaking a Masters of Arts in Kiswahili and Communication . She defended her proposal entitled: **UCHANGANUZI WA TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA: MFANO PARADISO.** She is due to collect data and l therefore request that she is accorded the necessary assistance.

Yours faithfully

Dr. Rose Mavisi
HoD Languages,Literature and Communication
Catholic University of Eastern Africa

THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA (CUEA) P.O. BOX 62157 00200 Nairobi – KENYA
Tel: 020-2525811-5, 8890023-4, Fax: 8891084, Email: admin@cuea.edu, Website: www.cuea.edu
Founded in 1984 by AMECEA (Association of the Member Episcopal Conference in Eastern Africa)

KIAMBATISHO II: Kibali cha NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **321221**

Date of Issue: **06/March/2026**

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Ms.. FRANCINE ADHIAMBO OCHARO of Catholic University of Eastern Africa, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: UCHANGANUZI WA TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA: MFANO PARADISO for the period ending : 06/March/2027.

License No: **NACOSTI/P/26/4186212**

321221

Applicant Identification Number

Ag. Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

KIAMBATISHO III: FOMU YA UCHANGANUZI WA DATA

Na.	Dondoo kutoka katika matini	Ukurasa	Lengo la utafiti	Kipengele kinachochanganuliwa	Mhimili wa Udenguzi	Tafsiri/Uchanganuzi wa mtafiti
1						
2						
3						
4						
5						
6						
7						
8						
9						
10						